# MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAULIDI YA JAMBENI

NA

CLARIS. U. CHANIRO

NAMBARI YA USAJILI: C50/ 76674/ 2014

TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KISWAHILI

KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

IDARA YA KISWAHILI

NOVEMBA, 2017

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

____________________________ _______________________________

Claris Uchi Chaniro Tarehe

( mtahiniwa)

NAMBARI YA USAJILI C50/76674/2014

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

_________________________ _______________________________

**Prof. Mohammed Abdulaziz** Tarehe

**(Msimamizi)**

________________________ ___________________________________

**Prof. Kinene wa Mutiso** Tarehe

**( Msimamizi)**

_____________________ ____________________________________

**Prof. Rayya Timammy** **Tarehe**

**( Msimamizi)**

## TABARUKU

Kazi hii nawatabarukia babangu Bw. Chaniro Chombo, mamangu Esther Chaniro, mume wangu Mwachizi Mwero, wanangu: Allan, Michael na Moses pamoja na kakangu Peter na dadangu Rachael. Mwenyezi Mungu awape heri njema maishani mwao.

**SHUKRANI**

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuniwezesha kukamilisha kazi hii kwa wakati ufaao. Vilevile nawashukuru wasimamizi wangu Profesa Abdulaziz Mohammed, Profesa Kinene wa Mutiso na Profesa Rayya Timammy kwa kunipa mwongozo thabiti na motisha katika kipindi hiki. Walinifaa sana katika kuisoma na kuirekebisha kazi hii hata ikakamilika. Mola awape afya njema na maisha marefu ili waendelee kuwaongoza wanafunzi wengine siku za usoni.

Shukrani nyingine ni kwa wahadhiri wafuatao katika idara ya Kiswahili, chuo kikuu cha Nairobi. Prof. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatia, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Prisca Jerono na Bwana Leonard Sanja. Waliniongoza katika kila hatua ya safari hii ya usomi na hata katika kufanya utafiti huu. Mola awabariki.

Shukrani zangu za dhati pia ziwaendee wanafunzi wenzangu tulioanza nao safari hii ya usomi kwa kuhimizana na kutiana motisha katika hali zote. Baadhi ya wanafunzi hawa ni: Ray, Florence, Lilian na Muinde. Nawatakia kila la kheri.

Pia namshukuru mume wangu, Bw. Mwachizi Mwero kwa msaada wake wa hali na mali wakati wa kipindi hiki cha usomi. Mungu ambariki sana. Sitawasahau watoto wangu: Allan, Michael na Moses kwa kunitia moyo na kunivumilia wakati wote wa masomo haya. Rabbana awahifadhi.

Mwisho namshukuru mwalimu mkuu Bw. Daniel Karanja pamoja na walimu wenzangu. Walinisaidia sana kwa kusimamia shughuli zilizohitaji uelekezi wangu nilipokuwa nikifanya utafiti huu. Mungu awatimizie haja za mioyo yao. Nitakuwa mtovu wa nidhamu kama sitamshukuru Bw. Wanga aliyepiga chapa kazi hii kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mola abariki kazi ya mikono yake.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| Bw. | Bwana |
| Dkt. | Daktari |
| Prof. | Profesa |
| S. A. W | Salla Allahu Wasalam ( Rehma na Amani Zimshukie Mtume) |
| Khj | Kama hapo juu |
| N.k | Na kadhalika |

**IKISIRI**

Utafiti huu umehusu uhakiki wa matumizi ya lugha katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni*. Malengo yetu ya utafiti yalikuwa ni kuchambua jinsi lugha ilivyotumika katika ukawafi huo, malengo mengine yamekuwa kuchanganua mbinu za matumizi ya lugha na jinsi zilivyochangia katika kufanikisha dhamira na maudhui katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni*. Tumetumia nadharia ya umuundo ambayo inatilia mkazo kwenye muundo wa kazi ya kifasihi. Utafiti wetu ulikuwa wa maktabani ambako tulikusanya data yetu na kuichanganua kwa maelezo. Vilevile tumefafanua baadhi ya vipengele vya kifani ambavyo mtunzi wa kazi yoyote ya kisanaa huvitumia katika kuwasilisha dhamira yake. Baadhi ya vipengele hivyo ni: muundo, mtindo na matumizi ya lugha. Aidha tumehakiki jinsi lugha ilivyotumiwa na mtunzi katika kufanikisha malengo yake katika hadhira lengwa. Tumechanganua tamathali za usemi na ambavyo zimejitokeza katika ukawafi tulioshughulikia. Mwisho tumeonyesha dhima ya tamathali hizo katika kuendeleza maudhui. Utafiti huu umebainisha kuwa lugha ni nyenzo kuu katika kupamba na kusisitiza ujumbe wa mtunzi. Hivyo mtunzi amefaulu kutumia lugha ya kitamathali katika ukawafi wake ili kuwasilisha dhamira yake.

## YALIYOMO

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAULIDI YA .......... 1

UNGAMO .......... i

TABARUKU .......... ii

SHUKRANI .......... iii

ORODHA YA VIFUPISHO .......... iv

IKISIRI .......... v

SURA YA KWANZA .......... 1

1.0 Utangulizi .......... 1

1.1 Tatizo la Utafiti .......... 3

1.2 Malengo ya Utafiti .......... 3

1.3 Maswali ya Utafiti .......... 3

1.4 Sababu za Kuchagua Mada .......... 3

1.5 Upeo Wa Utafiti .......... 4

1.6 Msingi Wa Kinadharia .......... 4

1.8 Njia Za utafiti .......... 13

Hitimisho .......... 14

SURA YA PILI .......... 15

UHAKIKI WA FANI KATIKA FASIHI .......... 15

2. 0 Utangulizi .......... 15

2. 1. Maulidi ya Jambeni .......... 15

2.2 Dhana ya Fani .......... 18

2.2.1 Matumizi ya lugha .......... 19

2.2.2 Muundo .......... 21

2.2.3 Mtindo .......... 21

Hitimisho ........ 22
SURA YA TATU ........ 23
UHAKIKI WA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAULIDI YA JAMBENI ........ 23
3.0 Utangulizi ........ 23
3.1 Matumizi ya Lugha ........ 23
3.1.1.1 Kiamu ........ 25
3. 1.2 Kiarabu ........ 26
3. 2 Tamathali za Usemi ........ 28
3. 2.1 Tashbihi ........ 29
3. 2.2 Sitiari ........ 31
3.2.3 Tashihisi ........ 33
3. 2.4 Chuku ........ 36
3.2.5 Takriri ........ 38
3.2.5.1 Takriri Irabu ........ 38
3.2.5.2 Takriri Konsonanti ........ 39
3.2.5. 4 Takriri Mzizi ........ 42
3.2.5. 5 Takriri Neno ........ 42
3.2.5.6 Takriri Wazo ........ 44
3.2. 6 Taharuki ........ 45
3.3 Jazanda / Taswira ........ 45
3.4 Lakabu ........ 50
3.5 Visawe ........ 51
3.7 Uhuru wa Kishairi ........ 53
3.7. 1 Ukiushi wa Kisintakisia ........ 53
3.7.2 Ukiushi wa Kisemantiki ........ 54

3.7.3 Ukiushi wa Kimofolojia ........ 55

3.7.3.1 Inkisari ........ 55

3.7.3. 2 Tabdila ........ 57

3.7.3. 3 Mazida ........ 58

3.8 Sajili ya Lugha ........ 58

3.8.1 Sajili ya Maabadini ........ 59

3.8.1.1 Sifa za sajili za Maabadani ........ 59

3.8.1.1.1 Uteuzi wa Msamiati Maalumu ........ 59

3.8.1.1.2 Matumizi ya Lugha ya Kuogofya na Lugha ya Matumaini ........ 61

3.8.1.1. 3 Matumizi ya maneno ya kigeni ........ 62

3.9 Dhima ya Matumizi ya Lugha katika Kuwasilisha Dhamira na Maudhui katika *Maulidi ya Jambeni* ........ 62

3.9.1 Kupamba Lugha ........ 62

3.9.2 Kufanikisha Mawasiliano ........ 63

3.9.3 Kufafanua Jambo ........ 64

3.9.4 Kuhamasisha Jamii ........ 64

3.9.5 Kumfikirisha Msomaji ........ 64

Hitimisho ........ 65

SURA YA NNE ........ 66

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 66

4.0 Utangulizi ........ 66

4.1 Muhtasari wa Utafiti ........ 66

4.2 Mapendekezo ........ 67

MAREJELEO ........ 68

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Katika utafiti wetu tumechambua jinsi lugha ilivyotumika katika *Maulidi ya Jambeni*. Maulidi haya yalitungwa na Muhamad Jambeni wa ukoo wa Al Bakari. Mtunzi ni mzaliwa wa mji wa Lamu. Maulidi haya yana beti tisini na tano ambazo zimegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inazungumzia ukoo wa Mtume, sehemu ya pili inazungumzia kuzaliwa kwake na utoto wake kwa jumla hadi kufikia wakati alipopewa utume. Sehemu ya tatu na ya mwisho inazungumzia safari ya Mtume kutoka Makka kwenda Madina.

Maulidi ni kisomo maalumu kinachosomwa ili kueleza maisha ya Mtume ( S. A.W), tangu kuzaliwa kwake. Ni sherehe ya kukumbuka siku aliyozaliwa Mtume Muhamad. Ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* unahusu historia ya kuzaliwa kwa Mtume Muhamad . Katika Maulidi haya tumeshughulikia jinsi lugha ilivyoteuliwa ili kuendeleza maudhui mbalimbali.

Nyenzo kuu ya kazi ya fasihi ni lugha. Mtunzi wa kazi ya kifasihi hawezi kuwasilisha dhamira na maudhui kwa wasomaji bila ya kuwako kwa lugha. Fasihi ni sanaa ambayo msanii hutumia ustadi wake katika kutumia maneno kiufundi ili kuwasilisha mawazo aliyonayo. Wamitila (2003) anakiri kwamba dhana ya fasihi ni ngumu kuifasili. Kimsingi fasihi ni kitu kilichoandikwa. Fasili hii haitoshelezi ufafanuzi kwa kuwa fasihi haiwezi kuandikwa katika ombwe tupu. Yanayowasilishwa katika fasihi lazima yatoe athari fulani kwa jamii husika. Hivyo maneno yanayowasilishwa kibunifu lazima yaguse na kuacha athari fulani kwa binadamu. Kazi hizi za kifasihi zinaweza kuwasilishwa kwa mdomo yaani fasihi simulizi au kwa kimaandishi, fasihi andishi. Utafiti wetu unahusu fasihi andishi. Katika fasihi andishi mtunzi ana njia nyingi za kuwasilisha ujumbe ambao ananuia kuuwasilisha kwa hadhira yake. Mwandishi anaweza kuwasilisha ujumbe kutumia riwaya, tamthlia, hadithi fupi au Ushairi. Mwanafasihi hutumia lugha kama nyenzo kuu kuwasilisha ujumbe wake. *Maulidi ya Jambeni* yameandikwa kwa kutumia ushairi.

Ushairi ni sanaa inayotumia lugha ya mkato ili kupitisha ujumbe ambao mtunzi ananuia kuuwasilisha kwa hadhira lengwa. Mtunzi wa mashairi huteua maneno kimaksudi ili kuleta

taswira fulani na mdundo wenye wizani. Njogu na Chimerah (1999 ) katika kufafanua dhana hii ya ushairi, wanaongezea kuwa maneno hayo ya mkato lazima yatumiwe kwa namna inayoathiri hisia za msomaji. Hisia hizi zinaweza kumfanya msomaji kudondokwa na machozi kwa mchomo wa maneno moyoni au kumliwaza na kumburudisha kwa maneno matamu ya kuliwaza. Mtunzi wa mashairi anapaswa kuteua maneno kiufundi ili yaweze kutoa mdundo fulani yanapoimbwa au kughaniwa. Kila shairi linapotungwa lazima mshairi awe na dhamira inayomsukuma katika utunzi wake ambayo ananuia kuiwasilisha kwa jamii husika.

Wanamapokeo Shaban Robert, Mathias Mnyampala na Abdilatif Abdalla, wanakubaliana kwamba ushairi ni utungo wenye ufasaha wa maneno ya hekima ambayo huandikwa kwa njia ya mkato kwa ulinganifu wa mizani na urari wa vina. Utungo huo pia huzua athari fulani kwa msomaji, (Senkoro, 1982).

Maelezo haya yanashabihiana na ufafanuzi wa Nyonje na Habwe (2007) ambao wanafafanua ushairi kama utungo wa kisanaa ambao ni mfupi unaopangwa katika mistari, mara nyingi inayoishia kwa vina. Wao wanaongeza kuwa shairi mbali na kuwa ni maneno yaliyoteuliwa kimakusudi, mtunzi pia hutumia wingi wa mbinu za kifasihi kama vile matumizi ya taswira, jazanda, sitiari, tashbihi na kadhalika.

Shairi tunalolishughulikia ni la bahari ya Ukawafi kama tulivyodokeza awali. Msokile ( 1993) anasema kuwa ukawafi ni aina ya shairi ambalo mishororo yake imegawanywa katika vipande vitatu yaani ukwapi, utao na mwandamizi. Katika kusisitiza maelezo haya, Wamitila (2003) anaafikiana na maelezo ya Msokile lakini anaweka nyongeza kuwa muundo huo wa vipande vitatu katika kila mshororo unafaa kuendelea katika shairi zima. Mbali na kuwa na muundo huo Njogu na Chimerah (1999) wanakubaliana na maelezo hayo na pia wanadokeza kuwa shairi la Ukawafi linaweza kuwa na mishororo mitatu, minne au hata mitano katika kila ubeti. Mizani ya vipande vya mishororo inaweza kuwa na mkondo wa sita kwa nne kwa tano, (6-4-5). Kumaanisha kuwa ukwapi uwe na mizani sita, utao mizani nne na mwandamizi mizani tano katika kila mshororo. Kawafi zingine zina muundo wa mizani 5-8-8. Tungo nyingi za Ukawafi zina vina vya ukwapi vinavyofanana katika kila ubeti lakini vina vya utao na mwandamizi

vinatofautiana. Ukawafi tunaouchanganua unafuata mkondo wa mizani sita kwa nne kwa tano. Pia una vina vya kipande cha ukwapi  na vina vya kipande cha mwandamizi vinavyofanana katika kila ubeti lakini vina vya utao ni tofauti katika kila mshororo.

### 1.1 Tatizo la Utafiti

Tatizo letu la utafiti ni kuchanganua jinsi lugha ilivyoteuliwa ili kuwasilisha dhamira na maudhui katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni*. Lugha ndiyo nguzo kuu katika kazi yoyote ya kifasihi. Mtunzi hana budi kuteua msamiati ambao unavutia na kunata makini ya msomaji ili kuwasilisha ujumbe. Mtunzi wa ukawafi huu, ametumia lugha ya kitamathali ili kusisitiza dhamira kuu. Tatizo letu ni kuchanganua matumizi ya lugha na jinsi yanavyochangia katika ufanisi wa kazi hii. Katika usomi wetu, tumebaini kuwa matumizi ya lugha katika *Maulidi ya Jambeni* hayajafanyiwa utafiti wowote wa kiusomi. Utafiti wetu unanuia kuziba pengo hilo.

### 1.2 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti wetu ni kuchanganua matumizi ya lugha katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni.* Malengo mengine:

(1) Kuchambua uteuzi wa matumizi ya lugha na mbinu nyingine katika ukawafi huu.

(2) Kubaini kama uteuzi wa matumizi ya lugha umechangia katika kuwasilisha ujumbe au kama hayakufaa katika kuwasilisha ujumbe.

### 1.3  Maswali ya Utafiti

(1) Mbinu za matumizi ya lugha zinazojitokeza katika ukawafi huu ni zipi?.

(2) Uteuzi wa matumizi wa lugha katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* umechangia vipi katika uwasilishaji wa ujumbe au kutowasilika kwa ujumbe.

### 1.4  Sababu za Kuchagua Mada

Tumechagua mada hii kwa sababu kadhaa. Kwanza, kipengele cha matumizi ya lugha hakijafanyiwa utafiti wa kiusomi katika ukawafi huu hivyo kuna upungufu wa kiusomi kuhusiana na tafiti za awali. Pia tulitaka kutambua tamathali za usemi ambazo mtunzi ametumia ili kuwasilisha maudhui yake, matarajio yetu ni kwamba kazi hii itawanufaisha watafiti wa baadaye pia watumizi wa lugha ya Kiswahili kwa jumla. Kwa kuwa tumechanganua lahaja

iliyotumiwa na mtunzi pamoja na maneno ya Kiarabu, hivyo itakuwa rahisi kwa wasomi wa kawafi kama hizi kuzielewa vyema.

### 1.5 Upeo Wa Utafiti

Utafiti wetu umejikita katika kuchambua jinsi lugha ilivyotumika katika *Maulidi ya Jambeni*. Tumesoma ukawafi huu kwa kina kisha tukachanganua mbinu za lugha zilizotumiwa na mtunzi na mchango wake katika kufanikisha kazi hiyo. Matumizi ya lugha ni mojawapo ya vipengele vya fani katika kazi za kifasihi ambavyo ni muhimu sana katika uwasilishaji wa maudhui na dhamira. Vipengele vya matumizi ya lugha tulivyochanganua ni pamoja na tamathali za usemi, lahaja iliyotumika, sajili ya lugha iliyotumiwa na mtunzi, taswira na majina ya kilakabu aliyoyatumia mtunzi kutokana na sifa za Mtume Muhamad. Hatukuchambua maudhui ijapokuwa tumeonyesha tu jinsi lugha ilivyotumiwa katika kukuza maudhui yake.

### 1.6 Msingi Wa Kinadharia

Katika utafiti wetu tumeongozwa na nadharia ya umuundo. Wamitila (2002) anasema kuwa nadharia hii inahusishwa na wanaisimu wa Shule ya Prague kabla ya kuanguka kwake. Kuzuka kwa shule hii kunahusishwa na wanaisimu wa Moscow walioathiriwa na wahakiki wa nchi za Zeshislovakia. Mawazo ya mwanaisimu Ferdinard de Saussure na Edmund Husserl ndiyo yaliyoweka msingi wa nadharia ya umuundo. Wana muundo kama vile Roman Jakobson walivutiwa na kiwango cha sauti katika ushairi; naye Jan Mukarovsky alichunguza suala la mizani katika ushairi wa Ki- Zeshi.

Uvamizi uliotokea huko Ujerumani wa miaka ya 1938- 1948 uliathiri shughuli za Shule ya Prague. Suala hili lilifanya baadhi ya wahakiki kama vile Roman Jakobson na Rene Wellek kutorokea Marekani. Utawala mpya wa Kikomunisti ulioendelezwa baada ya uvamizi huo ulisababisha uchunguzi wa kimuundo kupigwa marufuku. Jakobson na mwenzake waliyaendeleza mawazo yao walikotorokea.

Katika nadharia ya umuundo, mwanaisimu Ferdinard de Saussure aliweka msingi kwa kutofautisha kati ya matendo ya kiusemi na mfumo mpana wa lugha. Kulingana naye, tamko

lolote linalotamkwa na mtu fulani huwa na maana tu linapoangaliwa katika matumizi ya jumla ya lugha hiyo katika jamii husika. Katika mtazamo huu fasihi inachunguzwa kama njia fulani ya utumiaji wa lugha. Lugha ya kishairi kwa kiasi kikubwa ni tofauti na jinsi lugha ya kawaida inavyotumiwa kwa kuwa lugha ya kishairi huzichimuza ishara za lugha.

Katika uhakiki wao, wana muundo walizichunguza jinsi sauti, kiimbo, arudhi na utunzi wa mashairi unavyowiana katika tungo. Urejelezi wa nje wa kazi ya kifasihi haukufuatiliwa na wafuasi wa kimuundo bali lugha ndiyo inayotiliwa maanani sana. Lugha inaangaliwa kama mfumo unaojitosheleza ambao hautegemei jinsi mwandishi anavyokusudia katika uandishi wake.

Wahakiki wa kimuundo wanaamini kuwa viashiriwa havina maana na uzito zaidi kuliko viashirii. Hivyo wanatilia maanani jinsi maana inavyozushwa na kukuzwa na wala si maana inayojitokeza. Miundo ya kiuashiriaji hutiliwa mkazo katika kazi ya kifasihi kuliko maudhui. Kulingana na wana muundo, udhihirishaji wa muundo kwa jumla ndio unaoangaziwa zaidi.

Nadharia ya umuundo ina dhana ya ugatuzi wa nafsi, ambapo maana haitokani na mwandishi bali inatokana na sheria na kaida mbalimbali za mifumo tofauti ya kuashiria. Wamitila ( 2003) anasema kuwa katika ugatuzi wa nafsi, mwandishi na msomaji wa kazi husika, nafsi zao zinaondolewa katika uhakiki  hivyo kazi hiyo inachambuliwa kama huru. Nadharia hii inatilia mkazo mkubwa kwenye unasibishi wa maana wala si maana rejelezi. Maana nasibishi  ni maana inayohusishwa na neno wala si kile kinachorejelewa.

Wamitila ( 2003, 2008) anafafanua maana nasibishi kama maana inayojengwa katika akili ya msomaji inayotokana na uhusiano fulani wa neno. Nayo maana husishi ni maana inayorejelewa na neno lililosemwa. Kwa mfano neno fisi lina maana nasibishi ya mtu mlafi ilhali maana yake rejelezi ni mnyama. Mtunzi wa kazi ya kifasihi hutumia maana nasibishi ili kuwasilisha malengo yake katika hadhira lengwa.

Ntarangwi ( 2004)  analitaja neno kama ishara huru linaloelezwa kwa kutofautishwa na ishara nyingine. Lugha ni mfumo wa uhusiano kati ya viungo kadhaa, ni muundo sio kitu. De Saussure

alibuni dhana za kionyeshi ambacho ni lile neno na kionyeshwa ni dhana inayorejelewa na neno hilo. Dhana hizi mbili huenda pamoja na haziwezi kutenganishwa.

Umuundo wa lugha kwa kiasi kikubwa unaangazia vionyeshi na namna vionyeshi hivyo vinavyofanya kazi kuliko kuangalia nje ya mfumo wa lugha ambacho ni kinachoonyeshwa. Saussure alizingatia zaidi mfumo wa ndani wa lugha na si muundo wa nje. Mhakiki anayeangazia muundo wa lugha hufanya mtindo wa kazi kuwa kiini cha uhakiki wake.

Njogu na Wafula (2007) wakichangia katika nadharia hii ya umuundo, wanasema kuwa nadharia ya umuundo hupinga wazo la kijadi linalodai kuwa fasihi ni mchango wa maudhui na fani ambazo zinaweza kutenganishwa. Kulingana nao, kifasihi, mtindo unaweza kuainishwa na malengo ya msanii. Malengo ni dhamira aliyonayo mtunzi wa kazi ya kisanaa na mtindo ni namna dhamira zinavyowasilishwa. Umuundo unadai kuwa dunia ni umbo lisiloweza kugawika. Hivyo kuna viungo ambavyo lazima viungane ndipo viweze kutekeleza jukumu fulani.

Njogu na Wafula ( khj) wakimnukuu Ferdinard de Saussure (1959) wanadai kuwa lugha inayosemwa ina sehemu mbili zinazojidhihirisha. Kuna lugha dhahiri na lugha dhahania. Lugha dhahania huwa daima haibainiki wazi lakini hubainika katika mazungumzo ya kila siku na lugha dhahiri inadhihirika katika uwezo wa mtu wa kuunda sentensi kwa kadiri anavyoweza.

Mgullu (1999) anasema kuwa mfumolugha ( langue) ni mfumo dhahania ambao hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine katika jamii. Mfumo huu huundwa na vipashio vinavyohusiana kiuteuzi na kiusilisila. Uhusiano wa kiuteuzi unahusu uhusiano wa vipashio kiuamilifu. Uhusiano wa kiusilisila wa vipashio unahusu uhusiano wa kisarufi. Hivyo katika mpangilio wa maneno kisarufi, lazima mwandishi ateue maneno kutegemea sintaksia ya lugha inavyoelekeza. Mtaalamu huyu katika kufafanua dhana ya lugha, anakiri kuwa lugha ni mfumo changamano ambao una mifumo kadhaa ndani mwake inayotegemeana na kukamilishana. Mifumo hii ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Mtunzi wa kazi yoyote ya kifasihi lazima afuate sheria za lugha anayotumia ili kuunda sentensi sahihi

Kulingana na Saussure katika kitabu chake kilichochapishwa na wanafunzi wake ( 1959) anadai kuwa lugha ni mfumo wa alama ambazo zinajengwa na vijenzi viwili ambavyo ni kijenzi cha umbo sauti na kijenzi cha maana. Umbo sauti ni kiashiria cha umbo fulani na maana ya umbo sauti ndiyo kiashiriwa. Hivyo matumizi ya maneno yenye umbo sauti na maana hutoka kwa mfumo lugha. Neno ndilo umbo sauti kwani linajiwakilisha kwa namna tofauti tafauti. Kila alama inaashiria maana fulani na uhusiano huu wa kiashiria na kiashiriwa na wa kinasibu. Unasibu kulingana naye unamaanisha kuwa uhusiano uliopo kati yao si wa kisemantiki bali viashiria hupata maana zao zilizo tofauti na alama. Maana za alama hizo hutokana na jinsi jamii husika itakavyoamua vile itakavyoipa alama fulani jina lake. Kutokana na unasibu huu anakiri kuwa mfumo huu wa lugha una utata kwa mwingiliano wa alama zinazotumika.

Njogu na Wafula ( 2007) wanadai kuwa muundo wa fasihi una vipengele vinavyotegemeana na ambavyo vinaelezwa kwa muktadha wa vipengele vingine. Vitengo vya kisanii kama vile maudhui, ploti, wahusika, muktadha na lugha haziwezi kuelezwa kwa upekee wake bali lazima vitengo vingine vijumuishwe katika ufafanuzi wake. Kwa mfano katika kufafanua wahusika lazima ujumuishe lugha na hata ploti ya kazi husika. Hivyo nadharia hii ya umuundo inasisitiza vipengele vya kazi ya sanaa na jinsi vinavyohusiana na kukamilishana katika utungo wa kifasihi. Umuundo unaangazia jinsi sehemu zinavyofungamana katika sanaa. Kazi yoyote ya kifasihi inatakikana iwe na muundo unaojitosheleza, yaani iwe na vipengele kama vile msuko, wahusika, ploti na lugha ambavyo vinachangiana na hivyo kukamilisha kazi husika.

Mweri ( 2010) anasema kuwa lugha ni mfumo wa ishara nasibu ambao hutumiwa na binadamu katika mazungumzo ili kurahisisha mawasiliano na ishara hizi hutokea katika utaratibu maalum. Maelezo haya ya Saussure na ya Mweri yanaweka mkazo kwenye unasibishi wa kazi ya kifasihi ambapo mkazo mkubwa wa maana unahusishwa na neno wala si kinachorejelewa. Mhimili mkuu wa nadharia ya umuundo ni kwamba lugha huchukuliwa kuwa mfumo wa ngazi ya kwanza na fasihi ni mfumo wa ngazi ya pili kwa kuwa fasihi hutumia lugha. Mhakiki anayetumia muundo anachanganua jinsi lugha inavyotumiwa katika fasihi.

.

Mweri (khj) anasema kuwa Saussure ndiye aliyeweka msingi katika sarufi miundo. Kulingana naye, maneno yanayotumiwa yana uhusiano wa kiwima na kimlalo. Uhusiano wima katika sentensi ni jinsi kipashio kimoja kinavyohusiana na kipashio kingine katika muktadha maalum. Huu ni uhusiano wa maneno yanayotumiwa katika muktadha maalum na yale ambayo yanaweza kutumika badala ya maneno hayo. Uhusiano wa kimlalo ni uhusiano wa vipashio vinavyounda sentensi katika utungo. Hivi ni vipashio ambavyo vinategemeana na kukamilishana. Kila kipashio huwa kinategemea kingine na kimoja kikitolewa neno linakosa maana. Kwa mfano 'Juma anasoma' ni sahihi lakini huwezi kusema 'paka anasoma' kwani paka hawezi kusoma. Mtunzi wa kazi ya kifasihi pia analazimika kutumia maneno akifuata uhusiano uliopo baina yake. Katika ushairi, mtunzi ana uhuru wa kutofuata sarufi lakini pia lazima abadilishe muundo huo kwa kiwango fulani ili asipoteze maana na dhamira yake katika kazi anayoandika.

Obuchi na Mukhwana ( 2015) nao wanakubaliana na wataalamu wa awali waliofafanua nadharia ya umuundo. Wao wanamtaja Mswizi Ferdinard de Saussure kama baba wa isimu ambaye anadai kuwa lugha ni mfumo wenye muundo wake ambao ni tofauti na lugha nyingine. Kwa kawaida lugha zote zina ngazi nne kuu yaani, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kulingana na Saussure ngazi hizi ni tofauti katika kila lugha. Lugha mahsusi ina sauti zake ambazo hutumiwa kuunda maneno, tungo na sentensi zilizokamilika na zenye maana. Sauti hizi huwa tofauti na sauti za lugha nyingine. Aidha mofolojia, sintaksia na semantiki za lugha moja zinatofautiana na lugha nyingine.

Mbali na kufafanua dhana za mfumo lugha ( langue), matumizi lugha, ( parole) na ujumla lugha, ( langage) Mukhwana na mwenzake pia walifafanua lugha kidaikronia na kisinkronia kutokana na mawazo ya Saussure. Hizi ni dhana ambazo zinadhihirisha kuwa lugha hubadilikabadilika. Maneno mapya yanaundwa kila wakati ilhali maneno mengine yakipotea. Katika mtazamo wa kidaikronia, lugha huangaliwa kama chombo kinachobadilika kila siku.

Hivyo mtazamo huu huangazia mabadiliko ya lugha kufuatia mpito wa wakati. Kuwa lugha, kama vile binadamu na wanyama ni kitu chenye uhai ambacho hubadilikabadilika katika

viwango vyake. Mtazamo wa kisinkronia pia unahusu uchunguzi wa lugha kama ule wa awali tofauti ni kuwa, uchunguzi huu unajikita katika lugha mahususi. Mtazamo huu unachunguza muundo wa maneno na sarufi katika wakati fulani maalumu. Dhana hizi mbili zinaingiliana na kutegemeana.

Uhakiki wa kimuundo unahusu kuchambua na kubainisha kanuni za kimsingi zinazotawala uwekaji wa alama ili kuleta maana katika sentensi. Kwa mfano katika sentensi kuna sehemu mbili yaani kiima na kiarifu. Kiima mara nyingi huwa ni nomino au kiwakilishi chake na kiarifu hujumuisha kitenzi ndani yake. Hivyo kazi ya kifasihi huwa imeundwa kutokana na miundo kadhaa na kazi ya mhakiki ni kuangalia jinsi miundo hii inavyohusiana ili kuleta maana. Katika ushairi mtunzi anaruhusiwa kutumia uhusiano wa vipashio ambavyo haviafikiani ili kufuata arudhi za bahari anayoshughulikia.

Katika uhakiki wa kimuundo, mhakiki anachunguza muundo wa kazi nzima au sehemu ya kazi hiyo. Hivyo mhakiki anaweza kuhakiki muundo wa riwaya au sehemu yake na kama ni ushairi basi mhakiki anaweza kuhakiki kipengele kimoja katika shairi husika. Kwa mfano, mhakiki anaweza kuchunguza wahusika, lugha ilivyotumika, muundo na hata mandhari. Uhakiki huu pia unahusu uchanganuzi wa miundo ya tungo za kifasihi kwa madhumuni ya kuonyesha jinsi sehemu za tungo hizo zinavyowekwa pamoja ili kujenga kazi maalumu. kwa mfano, ili shairi la kijadi likamilike lazima kuwe na vitengo mbalimbali kama vile, maneno, mishororo, mizani, vina, beti na n.k.

Nadharia ya umuundo inatilia mkazo jinsi vipengele mbalimbali vya kifani vinavyoingiliana na kuungana katika ujenzi wa umbo la kazi ya kifasihi. Kwa kuangazia vipengele hivi basi nadharia hii imetufaa katika kuafikia malengo yetu ya utafiti. Nadharia hii kwa kuwa inasisitiza muundo wa kazi, imetusaidia kuchanganua maswala ya kifani na matumizi ya lugha ni kipengele kimojawapo cha fani. Uhakiki wa kazi unasisitizwa zaidi katika umuundo bila kuhusisha jamii na maswala mengine katika jamii. Wana nadharia wanaangalia jinsi maneno yanavyopangwa na kuhusiana ili kutoa maana. Uhusiano huu mara nyingine hukosa kuafikiana au si lazima uafikiane.

### 1.7 Yaloyoandikwa Kuhusu Somo hili

Kuna tafiti nyingi za awali ambazo zimetafitia mada kama hii yetu ya kuchambua matumizi ya lugha katika kazi za kifasihi. Matumizi ya lugha ni mgao mmoja wa kifani ambao hutumiwa na watunzi wa kazi za kifasihi ili kuwasilisha maudhui na dhamira zao katika jamii. Kazi tulizozipitia zina mchango mkubwa katika utafiti wetu.

Umwoyo (1997), ametafiti fani katika ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega. Mtafiti huyu ameangazia diwani mbili ambazo ni *Upisho wa Malenga* na *Dafina ya Malenga*. Utafiti wake umedhihirisha kuwa fani ni kipengele chenye mchango mkubwa sana katika kufafanua dhamira ya msanii. Utafiti huu umetufaa katika kuchanganua baadhi ya tamathali za usemi alizoziangazia katika utafiti wake. Baadhi ya tamathali za usemi alizofafanua ni tashibihi, sitiari, chuku, tashihisi na nyingine. Utafiti huu unalingana na mada yetu kwani matumizi ya lugha ni kipengele kimoja wapo cha fani tofauti ni kuwa sisi tumechambua matumizi ya lugha katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni*. Utafiti wake umetuelekeza katika kufafanua baadhi ya tamathali za usemi alizoziangazia.

Kisilu (2003), amechanganua mwingiliano wa fani na maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia ambapo alijikita katika diwani za *Mchezo wa karata* na *Bara Jingine.* Vipengele vya fani alivyoviangazia ni kama vile tashbihi, takriri, sitiari, taashira, maswali ya balagha na mbinu zingine. Vipengele hivi hivi ndivyo tumevishughulikia katika utafiti wetu. Utafiti huu umetuongoza katika kufafanua baadhi ya tamathali za usemi. Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kuwa sisi tumeshughulikia jinsi lugha ilivyotumiwa katika *Maulidi ya Jambeni.*

Mungai (2005), ameshughulikia fani katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* akilinganisha na *Utenzi wa Swifa ya Nguvu Mali*. Utafiti wake umetufaa kwani amefafanua vipengele vya matumizi ya lugha ambavyo tumevishughulikia katika utafiti wetu. Tofauti ya utafiti wake na wetu ni kuwa sisi tumechanganua matumizi ya lugha katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni.*

Wesa (2005), amehakiki uchambuzi wa fani katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.* Katika utafiti wake, vipengele muhimu vya kifani vilichanganuliwa kwa kina vikiwemo vipengele vya

matumizi ya lugha. Utenzi huu pia umejikita katika maswala ya kidini. Utafiti huu umetusaidia kufafanua tamathali za usemi ambazo mtunzi amezitumia ili kuwasilisha dhamira na maudhui yake. Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kuwa sisi tumechanganua matumizi ya lugha katika Ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni.*

Kofa (2006), amechanganua fani katika utenzi wa *Swifa ya Nguvu Mali*. Katika utafiti wake amechambua vipengele vya fani kama vile wahusika, mtindo, muundo na matumizi ya lugha. Katika utafiti huu mhakiki amefafanua kwa undani tamathali za usemi ambazo mtunzi amezitumia ili kusisitiza ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Utafiti huu umetufaa kwa kutuelekeza jinsi ya kubaini tamathali za usemi katika kazi ya kifasihi. Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kuwa, sisi tumechanganua matumizi ya lugha katika utenzi wa *Maulidi ya Jambeni.*

Mukuthuria (2007) amehakiki upekee wa utenzi wa *Swifa ya Nguvu Mali*. Katika uhakiki wake aliangazia jinsi mtunzi wa utenzi huo alivyotumia lugha katika kuendeleza dhamira na maudhui yake. Amefafanua tamathali kama vile jazanda, tashbiha, tanakuzi na takriri. Pia amefafanua jinsi tamathali hizi zilivyojitokeza na mchango wake katika kuendeleza lengo kuu. Utafiti wake umetufaa katika kubaini baadhi ya tamathali ambazo tumeziangazia katika utafiti wetu ambao umejikita katika *Maulidi ya Jambeni*.

Omari (2010), ameshughulikia uchambuzi wa tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Huu ni utafiti ambao umetuelekeza jinsi ya kuchunguza matumizi ya lugha kama vile sitiari, tashibihi, chuku na tamathali zingine za lugha. Tofauti ni kuwa sisi tumechambua matumizi ya lugha katika ukawafi wa *Maulidi ya jambeni*.

Lugwiri (2011), amechunguza sitiari, taashira na tashbihi katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*. Ameelezea dhana hizi tatu kwa kufafanua na kuonyesha aina zake na jinsi zimechangia kuendeleza dhamira na lengo la mshairi kwa hadhira yake. Kuna mbinu ambazo zilitumia wanyama katika ulinganishi wake. Kwa mfano, mtunzi katika utenzi huo ametumia simba akirejelea nguvu zake. Mnyama mbuzi pia amemtumia kulinganisha moja kwa moja na

watu wasio na mwelekeo katika jamii. Utafiti huu umetusaidia katika kuzifafanua dhana hizi katika ukawafi tunaoushughulikia. Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kuwa, sisi tumehakiki matumizi ya lugha katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni.*

Mwilaria (2011), ameshughulikia fani katika *Utenzi wa Ayubu.* Baadhi ya vipengele alivyo vishughulikia ni tamathali za usemi na wahusika. Amefafanua mbinu za tamathali kwa kina na kuonyesha jinsi zinavyochangia katika kuendeleza ujumbe kwa hadhira. Vile vile utafiti huu umetupa mwongozo katika kupambanua baadhi ya tamathali za usemi tulizozishughulikia katika kazi yetu ambapo sisi tumehakiki matumizi ya lugha katika ukawafi tunaoshughulikia.

Ndumbu (2013) amefanya uhakiki wa matumizi ya takriri na sitiari katika *Utenzi wa Rasil Ghuli*. Utafiti huu umetusaidia kubainisha jinsi takriri na sitiari zinavyojitokeza katika kazi ya kifasihi. Mhakiki huyu ameangazia namna mbinu hizi zinavyochangia katika kuleta mnato na kufanya msomaji awe na hamu ya kutaka kuendelea kuisoma kazi husika. Utafiti huu unawiana na wetu kwani sitiari na takriri ni baaadhi ya vipengele vya matumizi ya lugha ambavyo tumevichanganua katika utafiti wetu. Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kuwa, sisi tumehakiki matumizi ya lugha katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni.*

Kombo (2014), amehakiki tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini. Utafiti huu umeangazia baadhi ya tamathali za usemi zinazotumiwa katika mashairi ya ukimwi magazetini. Tamathali alizozifafanua ni taswira, sitiari, takriri, tasfida, tashibiha na ishara. Mtunzi ametumia tamathali hizi ili kubainisha dhamira zinazojengwa na lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini. Utafiti huu umetusaidia kutuongoza katika kubainisha tamathali hizi katika *Maulidi ya Jambeni*.

Karanja ( 2014) amechanganua matumizi ya sitiari, tashbihi na taashira katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Katika utafiti wake amefafanua tamathali hizi kwa kina na kuziainisha katika aina mbalimbali. Aidha ameonyesha jinsi tamathali hizi zilivyojitokeza katika diwani hiyo na jinsi zilivyochangia katika kufanikisha dhamira ya mtunzi. Utafiti huu umetufaa katika kutuongoza jinsi ya kufafanua tamathali hizi katika ukawafi tulioshughulikia.

Faki (2015), amehakiki sifa za kifani za utendi wa Kiswahili akitoa mfano wa *Utendi wa Fumo Liyongo*. Katika utafiti wake amechanganua tamathali za usemi kama vile taswira, maswala la balagha, kinaya, sitiari, tashibha na vipengele vingine. Vipengele hivyo vimetumika kwa ufundi wa hali ya juu kuhakikisha kwamba utenzi huo unakuwa na mvuto kwa wasomaji na wasikilizaji wake. Utafiti huu umetufaa katika kuchanganua tamathali za usemi katika utafiti wetu. Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kuwa sisi tumechanganua matumizi ya lugha katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni*.

Muchiri (2016) amehakiki fani katika *utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walli*. Katika utafiti wake amechanganua vipengele vya fani ambavyo ndiyo nguzo kuu ya kazi ya kifasihi. Vipengele alivyovifafanua ni msuko, muundo, mandhari, wahusika na uhusika, na matumizi ya lugha. Katika kipengele cha matumizi ya lugha amefafanua baadhi ya tamathali za usemi kama vile maswala ya balagha, tashibihi, takriri, chuku, taswira, uzungumzi nafsia, misemo na mbinu nyinginezo. Aidha amefafanua jinsi vipengele hivi vilivyojitokeza katika utenzi huo. Utafiti huu ni sawa na utafiti wetu kwani sisi tumechanganua matumizi ya lugha zikiwemo tamathali za usemi katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni*.

Soud (2016), amehakiki fani katika *Maulidi ya Nuni*. Utenzi huu umefafanua siku aliyozaliwa Mtume Mohammad na maisha yake kwa jumla. Mhakiki huyu amechanganua vipengele vya kifani kama vile mandhari, muundo wa kazi, tamathali za usemi kama vile takriri, tashbihi, sitiari, chuku n.k. Utafiti huu umetufaa sana katika utafiti wetu kwani unazungumzia swala kama letu lenye dhamira na maudhui mamoja. Utafiti huu unatofautiana na utafiti wetu kwa kuwa sisi tunachanganua matumizi ya lugha katika *Maulidi ya Jambeni* wala si *Maulidi ya Nuni*.

## 1.8 Njia Za utafiti

Utafiti wetu unahusu fasihi andishi katika utanzu wa ushairi. Hivyo tumejikita katika utafiti wa maktabani. Tumesoma *Maulidi ya Jambeni* ambayo yana beti tisini na tano, ili kuyaelewa kwa undani kwa lengo la kuchanganua matumizi ya lugha yaliyotumiwa na mtunzi ili kuwasilisha dhamira na maudhui yake.

Pili, tumesoma kazi za watafiti waliotangulia zinazohusu mada yetu tunayoishughulikia, hasa zilizojikita katika vipengele vya fani ikiwa matumizi ya lugha ni miongoni mwa vipengele hivyo. Tatu, tumetafuta ushauri kutoka kwa wasimamizi wetu, ili kupata mwongozo mwafaka kuhusu mada ya utafiti. Aidha tumewajumuisha wahadhiri wa fasihi na isimu ili kupata mchango wao kwa madhumuni ya kupata mwelekeo zaidi.

Mtandao pia ni njia muhimu katika utafiti wetu. Tumedurusu mtandao ili kupata maelezo kuhusu nadharia tuliyoitumia na yaliyoandikwa kuhusu mada hii. Data tuliyoikusanya tumeichanganua na kuifafanua kwa njia ya maelezo.

**Hitimisho**

Maulidi ni sherehe ambayo huthaminiwa sana na waumini wa dini la Kiislamu. Sherehe hii huonekana kama sikukuu inayoleta heri katika jamii. Hivyo waumini husoma maulidi wanapofanya shughuli zao za kila siku. Husoma maulidi wanapoingia kwenye nyumba mpya, wanapotoka kwenye arobaini ya uzazi, wanaporudi kuhiji Makka, wanapotoa watoto jandoni, wanapoowa na kuolewa, wanapotoka eda na kadhalika.

## SURA YA PILI

## UHAKIKI WA FANI KATIKA FASIHI

### 2. 0 Utangulizi

Katika sura hii, tumetoa muhtasari wa *Ukawafi wa Maulidi ya Jambeni* na kufafanua msingi wa uhakiki wa kifani katika kazi ya kifasihi. Hivyo, tumechambua vipengele vinavyojenga fani katika uhakiki kama vile, matumizi ya lugha, muundo na mtindo.

### 2. 1. Maulidi ya Jambeni

Kama tulivyosema katika sura ya kwanza, *Maulidi ya Jambeni* ni utungo unaozungumzia kuhusu maisha ya Mtume Muhamad kutoka kuzaliwa kwake hadi alipofanya kazi yake ya kueneza dini. Mtume Muhamad alizaliwa mji wa Makka mwaka wa 571. Kabla Mtume kuzaliwa, Mola alimpa Bi. Amina ujumbe akiwa usingizini kuwa amepata ujauzito wa Bwana wa Heri. Aliahidiwa kuwa Mtoto anayemtarajia amwite jina la Muhamad maana yake ni aliyesifiwa na hapo ataona baraka zake Mola.

Jamii ya Makka ilikuwa na desturi ya kuwachukuwa watoto wao na kuwapeleka kijijini kulelewa huko kwani waliamini malezi ya kijijini yalikuwa na hewa safi na bora zaidi kuliko malezi ya mjini. Hivyo Mtume akachukuliwa na Bi. Halima kwenda kumlea kijijini kwa muda wa miaka minne.

Mtunzi katika *Maulidi ya Jambeni*, anatufahamisha kuwa mwaka huohuo Mtume aliporudishwa na Bi. Halima kwa mama yake, walienda safari kuelekea Madina ambako kwa bahati mbaya, Bi. Amina aliaga dunia pindi tu aliporudi Makka. Tukio hilo lilimfanya Mtume kuwachwa mikononi mwa babu yake Bwana Abdul- Muttalib ambaye naye aliaga dunia miaka miwili baadaye.

Yalipotimiya myaka mine umri wake,
Alishika ndiya kasafiri naye mamake,
Aka azimiya munawari ili wafike,
Kirudi mamake ikawele ndiyo hatima.
(ubeti wa 40).

Babu pia aliondoka duniani na alibaki na ami yake bwana Abu Talib ambaye waliishi naye hadi alipopata familia yake. Abu Talib alikuwa na mazoea ya kusafiri naye kwenye misafara ya kibiashara na hapo ndipo alipopata fursa ya kuonana na Bi. Khadija ambaye baadaye ndiye aliyekuwa mkewe wa kwanza. Bi Khadija alikuwa na umri mkubwa kushinda Mtume kwani tayari alikuwa ashaolewa na mume mwingine. Mwenyezi Mungu aliibariki ndoa yao na watoto sita, wawili wa kiume na wakike wanne.

Mtume hakupendezwa na dini wanajamii wa Makka waliokuwa wakiabudu; wao waliabudu masanamu waliyojitengenezea. Hivyo yeye alikuwa na mazoea ya kwenda jabali Hira maili tatu kutoka Makka ambako alikuwa akimuabudu Mungu mmoja. Usiku mmoja akiwa pangoni, Malaika jibril alimtokea akiabudu. Malaika huyu alimwita Mtume mara tatu akimwagiza asome lakini kwa sababu hakuwa na utaalamu wa kusoma na kuandika, alimjibu Malaika kuwa yeye hakujua kusoma, hivyo si msomaji. Malaika hakumuacha aliendelea kumlazimisha na baadaye yeye Jibril alimsomea ujumbe huo, (ubeti wa 57).

Kija Jibrili, kwa utumwa wa Mola wake,
Hata kwa Rasuli, na hali yu pweke yake,
Katika jabali, li- Hiraa mahala pake,
Ili atamuke, ikira’a kwa kuisoma.

Huu ndiyo ufunuo ( wahyi) ambao Mtume aliupata na baada ya hapo akaanza kazi yake ya kueneza dini. Katika shughuli zake za utume, Mtume alikumbwa na shida nyingi sana. Mtume na maswahaba wake walivunja masanamu ya makafiri kitendo ambacho hawakukifurahia. Wengi walimpinga lakini Mwenyezi Mungu alimhimiza akariri Shahada, nguzo ya kwanza ya waislamu inayowaongoza. Nguzo hii ni ushahidi wa imani kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu (Allah) na kwamba Muhamad ni Mjumbe ( Mtume) wa Mwenyezi Mungu, ( ubeti 60).

Akapata shida T’umwa wetu akisimama,
Wapije shahada masanamu kuyasukuma,
Washike ‘ibada aloyeta Mola Karima,
Kulla mtu mwema kaongoka na kumwandama.

Mwaka wa 621, Mtume alifiwa na mkewe Bi. Khadija na baadaye ami yake aliyemlea pia aliaga dunia. Mwaka huu ulikuwa mwaka wa huzuni kwa Mtume kwani aliwapoteza wapendwa wake. Mwenyezi Mungu alipoona huzuni na masikitiko ya Mtume, alitaka kumfariji. Rabbana alimuagiza Malaika Jibril ampeleke Mtume kwenye safari ya ajabu ili asahau yale yaliyotokea. Jibril alimchukua Mtume kutoka msikiti wa Makka hadi msikiti wa Makadasi ulioko Jerusalem. Safari hiyo ilikuwa ya usiku mmoja na walitumia mnyama buraki ambaye ni mdogo kuliko farasi na mkubwa kuliko punda. Safari hiyo iliwafurahisha Mitume hadi wote wakashuka na kuswali naye rakaa mbili. Hapa ndipo alipochaguliwa kuwa imamu. ( ubeti 64 ).

Akisa kufika, Makadasi msikitini,
Mtumi kushuka, walitoka wote mbinguni,
Amri katoka, wakaswali raka 'ateni,
Na wetu amini, akawekwa kuwa imama.

Safari hii pia imeandikwa katika Qurani takatifu 17:1

" Utukufu ni wake yeye ambaye alimpeleka mja wake usiku
( mmoja tu ) kutoka msikiti mtukufu wa Makka mpaka msikiti
wa mbali (wa Baytul Muqaddas-Falastin) ambao (tumeubariki na)
tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake. (Tumempeleka hivyo)
ili tumuonyeshe baadhi ya Alama zetu. Hakika Yeye
( Mwenyezi Mungu) ni mwenye kusikia na mwenye kuona.
( Kurani sura ya 17, Surat Bani Israil :1 )"

Pindi tu walipomaliza kuswali, ngazi ilishuka na Jibril akaja kumwambia Mtume apande kwenda kwa Rahamani wake kwani yeye (Mtume) ndiye kipenzi chake. Mtume alipanda bila uoga wowote hadi mbingu ya saba. Mola alimwambia Mtume aombe chochote kutoka kwake naye atampa. Baadaye alitembezwa Jahanamu na kujionea jinsi wanaotenda maovu watakavyoadhibiwa siku ya kiyama na alipofika peponi aliona mahurulaini waliotayarishwa kwa wanaume wanaoishi maisha matakatifu ulimwenguni, (ubeti 68 na 69). Katika safari hiyo, Mtume alipewa swala ambazo mwanzoni zilikuwa hamsini lakini kwa huruma ya Mwenyezi Mungu swala hizo zilipunguzwa hadi tano. Swala hizi zilidhamiria kuwaongoza waumini katika kumshukuru Rabbana, kumtukuza na pia kuomba mahitaji yao ya kila siku.

Mtume aliposhuka kutoka mbingu hizo, aliwaelezea wanajamii wa Makka kuhusu safari yake ya usiku, wengi hawakumuamini bali walimkejeli na kumcheka. Jamii ya Ansari, wake kwa waume waliamua kufuata dini ya Mtume. Makuresh hawakufurahia jinsi Mtume alivyotangaza kuwa yeye ni Mtume wa Mungu na kuwa wanafaa kuabudu Mungu mmoja waache tabia zao za kuabudu masanamu. Hivyo walipanga njama ili wamuangamize na pia waiuwe dini yake, lakini Mungu kwa kuwa ana uwezo mkuu hata wakuona mambo ya siri, alimuagiza Mtume ahame mara moja na kwenda mji wa Madina, (ubeti wa 74). Bado Makureish walimfuata safarini ili kumuua hata wakaweka ahadi kuwa atakayemuua Mtume atapewa zawadi ya ngamia mia moja. Surata alishikwa na tamaa hivyo akaamua kuwafuata ili amuuwe Mtume lakini Mwenyezi Mungu alifanya muujiza wa kukwamisha farasi wake mchangani. Kila alipotaka kumfuata Mtume, farasi wake alizama tena mchangani. Mwisho aliomba msamaha na kujiunga na dini ya Mtume. Walifika Madina salama salimini, maelezo haya yanajitokeza katika ubeti wa 74.

T'umwa akatoka kwa amri yake Moliwa,
Akagura Maka na Madina akapokewa,
Dini katukuka ndipo hapo ilipokuwa,
Na wote wakawa makafiri kurudi nyuma.

## 2.2 Dhana ya Fani

Fani ni namna msanii anavyofinyanga kazi yake ili kuelezea hisia na mawazo yake kwa ufasaha. Katika fasihi, hivi ni vipengele ambavyo msanii anavitumia ili kueleza maoni yake kwa njia ya ubunifu. Waititu na Ipara (2006) wanafafanua dhana ya fani kama kipengele cha ushairi kinachotumiwa na mtunzi ili kuwasilisha maana aliyokusudia. Vipengele hivi vinawekwa na mtunzi wa kazi husika kwa mpangilio maalum. Baadhi ya vipengele vya kifani ni muundo, mtindo, matumizi ya lugha na wahusika.

Wamitila ( 2003) anaifafanua fani kama dhana ambayo hutumiwa ili kuonyesha muundo na jinsi kazi ya kifasihi ilivyopangwa. Wahakiki wa kifani huelezea mbinu na mtindo anaotumia mtunzi ili kuuwasilisha ujumbe wake. Kwa upande wake Mulokozi (1996) anafafanua fani kama vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii ili kufikisha ujumbe kwa hadhira yake. Kazi yoyote ya kifasihi huwa na sehemu mbili muhimu ambazo ni

sehemu ya fani na maudhui. Maudhui ni yaliyomo katika kazi ya fasihi, maswala yanayozungumziwa katika kazi husika. Fani ni kipengele cha kisanaa kinachotumiwa ili kuwasilisha maswala yanayozungumziwa katika kazi hiyo. Bila fani, maudhui hayawezi kuwasilishwa. Utafiti wetu unashughulikia kipengele kimoja cha fani ambacho ni matumizi ya lugha katika *Maulidi ya Jambeni.*

Njogu na Chimerah ( 1999) wanafafanua fani kama ufundi wa kisanaa ambao mtunzi wa kazi yoyote ya kifasihi huutumia ili kuwasilisha ujumbe wake. Vipengele muhimu vya kifani vinavyohakikiwa katika kazi ya kifasihi ni lugha, muundo, wahusika na mtindo. Mbatiah ( 2001) kwa upande wake anaifafanua dhana ya fani kama vipengele vya kimtindo vinavyojenga kiunzi kinachobeba ujumbe katika kazi ya kifasihi. Hata yeye anakubaliana na maoni ya Mulokozi kuwa kazi yoyote ya kifasihi huwa na sehemu mbili yaani maudhui na fani. Maudhui yakiwa maswala makuu yanayoshughulikiwa katika fasihi. Fani ni njia inayotumiwa kuyawasilisha maswala hayo. Sisi tunakubaliana na maoni ya wataalamu hawa kuwa fani ni jinsi mtunzi anavyofinyanga lugha ili kuwasilisha dhamira yake.

Mawazo ya wataalamu hawa yanaungwa mkono na Msokile ( 1993) ambaye naye anaongezea kusema kuwa fani ndicho kipengele kinachoonyesha ufundi wa kisanaa katika kazi ya kifasihi. Hiki ndicho chombo kinachotumiwa na mtunzi ili kuwasilisha ujumbe kwa wasomaji wake. Vipengele vya kifani hutegemeana na kuathiriana na maudhui. Uhodari wa mtunzi katika utungaji wake hutegemea jinsi kazi yake inavyovutia kwa hadhira yake. Jinsi mtunzi anavyotumia vipengele vya kifani kwa ustadi huwezesha kazi yake ipendeze au kuwa chapwa kama hatatumia vipengele hivyo vizuri.

Utafiti wetu unahusu uchambuzi wa matumizi ya lugha katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni.* Lugha ni kipengele kimojawapo cha fani. Katika kuwasilisha maudhui na dhamira katika fasihi, mtunzi lazima ateue lugha yenye mnato na inayovutia wasomaji wake na kuwapa hamu ya kuendelea kutaka kuisoma ili kupata dhamira lengwa.

### 2.2.1 Matumizi ya lugha

Wamitila, (2003, 2004, 2008) anasema kuwa lugha ni udongo wa kufinyanga na kuuwasilisha ushairi. Lugha hutumiwa na mtunzi ili kujenga hisia na kuifanya hadhira ivutiwe, iburudike, pia

inaweza kuchomwa kwa lugha ya kuchoma au kuburudisha kwa kutumia maneno matamu. Anaendelea kusema kuwa lugha ndiyo nyenzo kuu ya kazi yoyote ya kifasihi. Lugha hii huundwa na msamiati ambao ni jumla ya maneno yapatikanayo katika lugha itumiwayo na mtunzi. Lugha ina nafasi kubwa katika fasihi kwa kuwa fasihi yenyewe ni sanaa ya lugha. Hii ndiyo nguzo kuu ya kazi ya kifasihi na uchunguzi wowote wa kazi hizo hauna budi kuangalia suala la lugha. Sanaa ya ufinyanzi na uchoraji hutofautishwa na sanaa ya fasihi kwa kuwa sanaa hizi hazitumii nyenzo ya lugha. Fasihi huitumia lugha kwa namna maalum inayozua lugha ambayo inajulikana kama lugha ya kifasihi.

Matumizi ya lugha katika kazi yoyote ya kifasihi hujitokeza kutegemea mambo mbalimbali ; kwanza uteuzi wa kipekee wa maneno huzua athari na picha maalum akilini mwa msomaji. Hizi ni athari ambazo zinaweza kumfurahisha au kumhuzunisha msomaji. Pia huwa na matumizi ya tamathali za usemi kama vile tashibihi, sitiari, takriri, kinaya na kadhalika ambazo humsaidia mtunzi kuafikia dhamira yake katika utunzi wake. Mtunzi pia huwa na uhuru ambao unamruhusu kutumia maneno ya miundo isiyo ya kawaida. Baadhi ya mbinu hizi ni mazida, inkisari, tabdila, bila kubadilisha maana ya neno lililotumika.

Katika utafiti wetu, kazi tunayoishughulikia ni ya ushairi, hivyo mtunzi amejikita katika sheria za utanzu huo. Lugha ya kishairi ina mpangilio maalum ambao unatofautisha shairi na kazi zingine za kinathari. Baadhi ya mashairi hupangwa katika vifungu yaani beti, kila ubeti huwa umegawika katika mishororo kulingana na bahari ya shairi hilo. Maneno katika ushairi hutumiwa na mtunzi kwa mpangilio maalum ili kuwasilisha ujumbe wake. Mshairi ana uwezo wa kuzungumzia mambo mengi akitumia maneno machache kwa muhtasari. Uwezo huu unatokana na jinsi anavyokubalika kutumia zana mbalimbali za lugha hasa zile zinazohusu tamathali za usemi.

Senkoro (1982) anasema kuwa mzizi wa kazi ya fasihi ni matumizi ya lugha na hutumiwa na mtunzi wa kifasihi ili kuyaibua mawazo yake na kuonyesha ukomavu wake katika kazi husika. Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* mtunzi ameteuwa msamiati mwafaka ili kuuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Mtunzi ni mzaliwa wa mji wa Lamu, hivyo ametumia lahaja ya Kiamu kwa kiwango kikubwa. Mbali na lahaja hii, pia ametumia maneno ya Kiarabu katika kazi yake.

### 2.2.2 Muundo

Kipengele hiki cha kifani huelezea muundo wa nje wa kazi ya kifasihi. Hii ni sura ya nje ya shairi ambayo inatengenezwa na mfuatano wa idadi ya beti, mpangilio wa vina, idadi ya vipande katika kila ubeti, pamoja na urari wa mizani na vina. Mashairi ya Kiswahili yana miundo mingi ambayo aghalabu hutegemea aina ya shairi. Muundo unaweza kuathiri kiini cha maana ya shairi na mtiririko wa shairi hilo.

Wamitila ( 2003) anaainisha kipengele hiki katika makundi mbalimbali. Kulingana naye kuna muundo pindu, muundo wa kiduara, muundo wa kidrama, muundo wa kivitushi, muundo wa ndani na muundo wa nje. Muundo pindu anauelezea kama muundo wa kifasihi ambao hutumiwa kupindua kauli fulani katika uhakiki wa kazi ya fasihi. Muundo wa kiduara ni muundo ambapo mtunzi anaonyesha sehemu ya mwisho ya hadithi ambayo ilikuwepo mwanzoni mwa hadithi hiyo. Muundo wa kidrama hutumiwa katika fasihi kuelezea hadithi za kitanzia ambazo zinamuangazia mhusika mkuu na mpinzani wake katika mgogoro wao na mfuatano wa matukio.

Muundo wa ki- vitushi ni muundo ambao unafafanua vihadithi ndani ya hadithi kuu lakini kuna viungo vinavyoviunganisha. Hadithi hizi zinaweza kuunganishwa na kiungo kama vile dhamira na motifu. Sehemu za ndani za kazi ya kifasihi huelezewa na muundo ndani ambapo kazi husika inaelezea jinsi sehemu za kazi hiyo zinavyohusiana na kutegemeana. Kwa mfano jinsi wahusika wanavyohusiana na maudhui na n.k. kazi ya nje ya hadithi huelezewa na muundo nje.

### 2.2.3 Mtindo

Kipengele hiki kinahusishwa na tabia ya utungaji ambao hupambanua mtunzi mmoja na mwingine. Hii ni jinsi mtunzi anavyotunga kazi na kuipa kazi hiyo uzuri kifani na kimaudhui. Kipengele hiki huelezea jinsi mtunzi anavyoteua msamiati wake, lahaja anayotumia katika kazi hiyo, matumizi ya nahau na misemo. Wamitila ( 2004) anasema mtindo ni njia ya kuiwasilisha tajriba ya mtunzi kwa kuupanga na kuuwasilisha welewa wake kwa jamii. Waititu na Ipara (2006) wanakubaliana na Wamitila kuwa mtindo ni kipengele cha kifani ambacho mtunzi hukitumia ili kuipa kazi husika sura inayoitofautisha kazi moja na kazi nyingine.

**Hitimisho**

Katika sura hii, tumejadili dhana ya fani na vipengele vya kifani vinavyotumiwa na mtunzi katika kuwasilisha dhamira. Kwanza tumetoa muhtasari wa ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* na kufafanua matukio muhimu yaliyotokea katika maisha ya Mtume Muhamad. Sura hii imetubainishia kuwa vipengele hivi ni muhimu na vinategemeana na kukamilishana katika utungo wowote wa kisanaa. Vipengele tulivyovijadili ni matumizi ya lugha, muundo na mtindo.

# SURA YA TATU

# UHAKIKI WA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAULIDI YA JAMBENI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tumejadili dhana ya fani na baadhi ya vipengele vya kifani ambavyo vinatumiwa na mtunzi kuwasilisha kazi yake. Katika sura hii, tumehakiki jinsi mtunzi wa maulidi haya alivyotumia lugha, lahaja aliyotumia tumeifafanua kwa undani na pia kubainisha sehemu maalum ambapo lahaja hiyo imetumiwa. Mtunzi ametumia lahaja ya Kiamu katika kuuwasilisha ujumbe wake. Aidha tumechanganua tamathali za usemi zilizojitokeza katika ukawafi huu na kuonyesha jinsi zilivyochangia katika kukuza maudhui. Tamathali za usemi tulizochambua ni tashibihi, sitiari, chuku, takriri, tashihisi na taharuki.

## 3.1 Matumizi ya Lugha

Kama tulivyosema katika sura ya pili, mtunzi wa kazi yoyote ya kifasihi hana budi kutumia lugha kujenga hisia na kuifanya kazi anayoishughulikia ivutie kwa wasomaji wake. Matumizi ya lugha katika fasihi huleta uzuri unaojitokeza kwa mitindo tofauti tofauti. Mtunzi huteua maneno yanayoleta athari na picha maalum. Pia, hutumia tamathali za usemi ambazo hupamba lugha na hata kusisitiza ujumbe unaowasilishwa. Mtunzi wa ukawafi tulioushughulikia ametumia baadhi ya maneno ya Kiarabu na lahaja ya Kiamu ili kuwasilisha ujumbe.

### 3.1.1 Lahaja

Odeo na Maliachi (2008) wanafafanua lahaja kama tofauti za kimatamshi na maumbo pamoja na matumizi katika lugha ambayo huhesabiwa ni moja ila hutofautiana katika mambo madogo madogo. Wanaendelea kufafanua lahaja za lugha kama namna mbalimbali za lugha moja. Hii ni dhana inayotumiwa ili kueleza lugha inayotumiwa na kikundi fulani cha watu ambapo tofauti za maneno, umbo na matamshi na aina nyingine za lugha fulani, (Wamitila 2003). Soud (2016) akimnukuu Crystal (1967), anafafanua lahaja kama mtindo bainifu wa lugha kieneo na kijamii unaobainishwa na seti maalum za maneno na miundo ya kisarufi.

Oriedo (2007) anafafanua dhana ya lahaja kama tofauti za jinsi maneno yanavyotamkwa na matumizi ya maneno haya katika asili moja au lugha moja. Mwilaria (2011) anasema lahaja ni matumizi ya kilafudhi ambapo jamii fulani hutamka maneno kulingana na watamkavyo wakaazi wa jamii hizo. Lafudhi hizo mara nyingi huongea Kiswahili kisicho sanifu. Watunzi wa kishairi aghalabu hutumia lahaja zao ili kutoa uhalisia wa ujumbe huu katika hadhira lengwa. Lahaja ni visehemu vya lugha mama, vinavyotumia kanuni za lugha zinazoshabihiana lakini si lazima kufanana. Tukimnukuu Kipacha (2003) anasema:

> "Lahaja ni matokeo ya lugha kuwa na launi kadhaa zinazowabainisha watumiaji wake mahali watokapo au tabaka lao. Tofauti za launi hizo haziadhiri maelewano baina ya mifumo na kanuni miundo ya lahaja hizo".

Wamitila (2008) kwa upande wake anafafanua dhana ya lahaja kama lugha inayotumiwa na kikundi fulani cha watu na huwa na tofauti za maneno, umbo na matamshi na aina nyingine za lugha fulani. Lugha ya Kiswahili ina lahaja mbalimbali. Baadhi ya lahaja hizo ni: Kimvita, Kiamu, Kingozi, Kiunguja, Kivumba, Kitikuu, Kisiu, Kijomvi, Chichifundi, n.k. Mtunzi wa *Maulidi ya Jambeni* ni mzaliwa wa mji wa Lamu na hivyo ametumia lahaja ya Kiamu katika kuwakilisha dhamira yake.

Mgullu (1999) anataja lahaja kama hali ambapo lugha moja inazungumzwa kwa namna tofauti tofauti lakini wazungumzaji wake wanaelewana japo kila mtu anatumia mtindo wake wa uzungumzaji. Kwa mfano lugha ya Kiswahili ina lahaja za Kaskazini na lahaja za Kusini ambazo zinatofautiana katika miundo ya maneno lakini wakizungumza wanaelewana. Baadhi ya lahaja za Kaskazini ni pamoja na Chimiini, Kibajuni, Kiamu, Kisiu, Kipate na Kijomvu. Baadhi ya lahaja za kusini ni Kipemba, Kiunguja, Kitumbatu, Kingazija, Kinzwani, Kimtang'ata na Kimakunduchi.

Kutokana na fafanuzi zilizotolewa na wataalamu hawa, ni dhahiri kuwa lahaja ni sehemu za lugha moja kuu ambazo zinafuata msingi wa lugha hiyo ingawa kuna tofauti za kimatamshi na kimsamiati kutokana na tofauti za kijiografia.

#### 3.1.1.1 Kiamu

Kiamu ni lahaja iliyo maarufu katika kisiwa cha Amu ( Lamu) na pambizoni mwake. Hii ni lahaja ambayo ina maneno mengi yenye asili ya kibantu na imehifadhi msamiati wake mwingi wa kale. Jina la Lamu lilitokana na jina la Kiarabu ‘ Bami Lami’ ambalo linatokea sehemu ya ghuba ya Uajemi, ( Somo na wenzake 2011).

Mtunzi katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutumia lahaja hii ili kuendeleza maudhui na malengo makuu katika kazi yake. Katika ubeti wa 94 anatudhihirishia kuwa yeye ni mkaaji wa mji wa Lamu na hivyo yuko tayari kufuata desturi na mila za mji huo ikiwemo lahaja inayotumiwa katika kisiwa hicho, (ubeti 94).

Na yangu kabila ni Bakari muifahamu,
Alonipa Mola kazaliwa nt’i ya Amu,
Ndiyo yangu mila ya mtumi mwenye hishima,
Nisake timami zake swifa zilo timama.

Lahaja hii imetumika ili ujumbe uweze kueleweka zaidi hasa kwa wanaotumia lahaja hiyo.
Lahaja ya Kiamu ina maneno ambayo yanatofautiana kifonetiki na maneno ya Kiswahili sanifu.

**Baadhi ya Maneno ya Kiamu yaliyojitokeza katika Ukawafi huu**

| Lahaja ya Kiamu | Kiswahili Sanifu | Ubeti | Tofauti za Kifonetiki |
|---|---|---|---|
| Nanda | Nanza | 1 | Sauti / nd / badala / nz / |
| Kundua | Kunjua | 6 | Sauti /nd/ badala /nj/ |
| Wanda | Wanja | 30 | Sauti / nd/ badala / nj/ |
| Vundika | Vunjika | 32 | Sauti / nd/ badala / nj / |
| Muyi | Mji | 91 | Sauti /y/ badala / j/ |
| Ndiya | Njia | 3 | Sauti /y/ badala /j/ |
| Yinalo | Jinalo | 1 | Sauti / y/ badala ya /j/ |
| Mayi | Maji | 34 | Sauti / y/ badala / j / |
| Yuu | Juu | 19 | Sauti /y/ badala / j / |
| Yambo | Jambo | 80 | Sauti /y/ badala / j/ |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kuyaa | Kujaa | 78 | Sauti / y/ badala / j / |
| Moya | Moja | 95 | Sauti /y/ badala / j/ |
| Kayeta | Kaleta | 50 | Sauti /y / badala / l / |
| Zombo | Vyombo | 78 | Sauti /z/ badala /vy/ |
| Zuo | Vyuo | 14 | Sauti / z / badala /vy/ |
| Zijana | Vijana | 95 | Sauti /z/ badala / v/ |
| Kyake | Chake | 6 | Sauti /ky/ badala /ch/ |
| Waswili | Wasili | 23 | Sauti / sw/ badala / s/ |
| Kitwa | Kichwa | 26 | Sauti / t / badala / ch / |
| Nti | Nchi | 94 | Sauti / t /badala / ch / |
| Mato | Macho | 81 | Sauti /t/ badala /ch/ |
| Kuteka | Kucheka | 37 | Sauti / t/ badala / ch/ |
| Wata | Wacha | 95 | Sauti /t/ badala /ch/ |
| Tukua | Chukua | 21 | Sauti /t/ badala /ch/ |
| Mwiso | Mwisho | 38 | Sauti /s/ badala / sh/ |
| Sharia | Sheria | 17 | Sauti /a/ badala /e/ |
| Alifu | Elfu | 92 | Sauti /a/ badala ya /e / |
| Nyee | Nywele | 83 | Sauti / ø/ badala / l/ |
| Mbee | Mbele | 44 | Sauti/ / ø/ badala /l/ |
| Lema | Jema | 22 | Sauti / l / badala / j / |
| Kuko | Huko | 26 | Sauti / k/ badala / h/ |
| Hini | Hii | 55 | Sauti / n/ badala /i / |

### 3. 1.2 Kiarabu

Lugha ya Kiarabu inahusishwa sana na waumini wa dini ya Kiislamu. Kiarabu ndiyo lugha iliyotumiwa kuandikia Qurani Takatifu ambayo maneno yake ni vigumu kutafsirika, hivyo hutoholewa ili yaweze kuonekana kama ya Kiswahili. Utenzi huu unazungumzia swala la dini ya Kiislamu, hivyo mtunzi hakuweza kuepuka utumizi wa maneno ya Kiarabu. Mtunzi katika Ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* amefanikiwa kutohoa baadhi ya maneno ya Kiarabu ili

kuwasilisha dhamira yake. Ukawafi huu unahusu maisha ya Mtume Muhamad, kiongozi wa dini ya Kiislamu. Mtunzi kwa kiasi kikubwa ameathiriwa na lugha ya Kiarabu, katika uwasilishaji wake. Tumeangazia baadhi ya maneno hayo na kutoa ufafanuzi wake kwa Kiswahili sanifu.

**Baadhi ya maneno ya Kiarabu yaliyojitokeza katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni***

| **Maneno ya Kiarabu** | **Kiswahili sanifu** | **Ubeti** |
|---|---|---|
| Rahima | Jina mojawapo la Mwenyezi Mungu kuashiria rehema na huruma zake | 29 |
| Jabbaru | Mwenyezi Mungu aliye mtawala mkuu wa kipekee | 28 |
| Shahada | Nguzo ya kwanza ya Kiislamu inayosema kuwa hakuna Mungu mwengine wa kuabudiwa ila Allah na Muhamad ni mtume wake | 60 |
| Ansar | Wafuasi wa Mtume waliokuwa Madina | 75 |
| Imamu | Kiongozi wa dini ya Kiislamu anayeswalisha swala ya jamaa. | 64 |
| Jibril | Malaika aliyepeleka ufunuo (Wahyi ) kwa Mtume | 57 |
| Mahurulaini | Viumbe wanawake wema wa Allah waishio peponi na ambao ni mabikira. | 25 |
| Wahyi | Ufunuo maalumu wa mambo ya siri za Kimungu ulioteremshiwa Mtume. | 57 |
| Rasuli | Mtume | 29 |
| Thenashara | Kumi na mbili | 43 |
| Swifa | Sifa | 35 |
| Himidi | Sifu | 3 |
| Burahimu | Ibrahim | 50 |
| Hijira | Safari ya Mtume kutoka Makka kwenda Madini | 93 |
| Mahashumu | Mheshimiwa kama Issa, Musa | 2 |
| Rakaa | Sehemu ya kitendo cha sala katika dini ya kislamu cha kusimama, kuinama na kusujudu. | 64 |
| Rakaa teni | Rakaa Mbili | 64 |

| | | |
|---|---|---|
| Ikra | Soma | 57 |
| Mola | Mwenyezi Mungu aliye muumba na Bwana | 90 |
| Nabia | Nabii aliye chaguliwa na Mwenyezi Mungu (mtume Muhamad) | 54 |
| Arsh | Kwenye kiti cha enzi cha Mola mtukufu. | 67 |
| Karim | Jina moja wapo la Mwenyezi Mungu aliye mkarimu | 60 |
| Kaaba | Jengo takatifu lenye umbo la mraba lililoko Makka na ambalo waislamu hulizunguka wakati wa kufanya ibada za Hijja | 52 |
| Rajab | Mwezi wa saba wa mwaka; mfungo kumi | 63 |
| Hamsa wa Ishirini | Miaka ishirini na tano | 46 |
| Mia teni | Mia mbili | 93 |
| Shaaban | Mwezi wa nane katika kalenda ya kiislamu; mwezi mmoja kabla ya Ramadhani | 93 |
| Alifu | Elfu | 93 |
| Rabbi | Mwenyezi Mungu | 94 |

### 3. 2 Tamathali za Usemi

Tamathali ni neno au fungu la maneno ambayo maana yake imefichwa. Katika kazi ya kifasihi matumizi ya tamathali ni muhimu sana katika kuifanya kazi iwe na msisitizo na mnato mkubwa kwa wasomaji wake. Tamathali za usemi ni matumizi ya maneno kwa namna fulani ili kuifanya lugha iwe ya kuvutia na kuifanya kazi ya sanaa iwe ya kupendeza.

Wamitila (2008) anafafanua tamathali za usemi ambazo zinahusisha ukiushi ambapo fungu la maneno linatumiwa na mtunzi kwa maana iliyo tofauti na maana ya kimsingi ya neno hilo. Mtaalamu huyu anatoa majukumu matatu makuu ya tamathali za usemi katika fasihi. Majukumu haya ni:

1. Kurembesha kile kinachozungumziwa na lugha hiyo ili kiwe na mvuto wa kisanaa.
2. Kufafanua kinachohusishwa na tamathali maalum.
3. Kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani.

Lugha ya kitamathali ni nyenzo muhimu katika ujengaji na uimarishaji wa hisia.

Mvati na wenzake (2009) wanasema kuwa tamathali za usemi ni mbinu katika kazi ya fasihi ambazo hutumiwa ili kuongeza maana kwenye lugha ya kishairi. Katika matumizi ya mbinu hizi, msomaji wa shairi anapata uelewa zaidi kuhusu ujumbe ambao unawasilishwa na mtunzi.

Msokile (1993) naye anaeleza tamathali za usemi kuwa ni semi ambazo mtunzi anatumia katika kazi yake ili kutia nguvu na kusisitiza maana, mtindo na sauti katika maandishi. Tamathali hizi hutumiwa ili kuipamba kazi ya sanaa na kuongeza utamu wa lugha. Mulokozi na Kahigi (1979), wanazielezea tamathali za usemi kuwa ni:

> ‘‘…..vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana dhahiri za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi kucheleweshа uelewa wa ujumbe alioufumbata katika kazi yake ya kisanaa’’

Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni*, mtunzi ametumia tamathali kadhaa katika kukuza maudhui makuu katika kazi yake. Tamathali tulizobaini ni tashibihi, tashihisi, sitiari, chuku na takriri na taharuki.

**3. 2.1 Tashbihi**

Wamitila (2003) anafafanua tashbihi kama ulinganishaji unaodhamiria kulinganisha sifa fulani na nyingine na kujenga picha ya aina fulani akilini kwa kutumia viungo kama vile: kama, mithili ya, mfano wa, sawa na, kama vile na ja. King’ei na Kemoli (2001) wanaifafanua dhana ya tashbihi kama ulinganishaji wa lugha. Mara nyingi, vitu vinavyolinganishwa huwa na mshabaha fulani wa sifa au tabia.

Msokile (1993) pia anachangia katika kuifafanua dhana hii, anadokeza kuwa tamathali hii hutumiwa ili kufananisha vitu vitatu ambavyo ni kizungumzwa, kifananishi na kiungo. Sisi tunakubaliana na maelezo ya wataalam hawa kuwa tashibihi ni mbinu inayofananisha vitu au sifa za kitu kimoja na kingine kwa kutumia viunganishi. Tashbihi hutumiwa na mtunzi ili kutilia mkazo jambo linalozungumziwa na pia kuirembesha lugha. Mbinu hii pia huitwa tashbisha au mshabaha.

Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni,* mtunzi ametumia tamathali hii ili kusisitiza mawazo yake. Katika ubeti wa 6, mtunzi anaeleza kuhusu kuzaliwa kwa Mtume Muhamad huku akimithilisha kizazi hicho kizuri na mkufu mzuri wa dhahabu uliotengenezwa na sonara.

Tena nakunduwa nguo njema uzazi wake,
Wa T'umwa moliwa ilo njema nasabu yake,
**Kama kya kufuwa kulla kyema kidani kyake,**
Hizo swifa zake kusikiwa ziwele njema.
( ubeti 6)

Mtunzi anapozungumzia kuzaliwa kwa Mtume, anasema kuwa mimba ya miezi tisa ilipotimia, Mtume alizaliwa. Kuzaliwa kwake kunamithilishwa na kutokea kwa mwezi mwandamo ambao husubiriwa kwa hamu na ghamu na waumini wa dini ya Kiislamu kabla ya kuanza mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani na ambao pia ndio wanaoutumia kujua mianzo ya miezi. Maelezo haya yanapatikana katika ubeti 24.

Yalipotimia mimba yake wetu Mungwana,
Ni myezi tisiya alizaa mwana Amina,
Ni mwana Asiya Mariyama walikutana,
**Akatoka Bwana kama mwezi waloandama.**

Mtume alienda safari ya usiku mmoja hadi mbingu ya saba akitumia ngazi kutoka msikiti wa baiti Mukadasi. Katika ubeti 67 Mtunzi anatufahamisha jinsi Mtume alivyokaribishwa na Mwenyezi Mungu kwa furaha. Ukaribu wa Mtume na Mola unamithilishwa na ukaribu wa Al kaaba na kile kitambaa cheusi kinachotumiwa kuifunika.

Akisikiya Arishini kwa Mola wake,
**Akakurubiya kama kandu na kaba yake,**
Mola kamwambiya utakalo kwangu utake,
Wewe ndiwe pweke niloumba mbingu Hashima.
( ubeti 67).

Katika kufafanua umbo la Mtume Muhamad, mtunzi anatuelezea harufu nzuri inayotoka mwilini mwake. Jasho lake ni kama manukato mazuri na jinsi anavyon'gaa mtunzi anamfananisha na lulu ambacho ni kito cha thamani kubwa sana. Mtume kila anapoweka mkono wake anaacha harufu nzuri inayozagaa kila mahali. Maelezo haya yanapatikana katika ubeti wa 84.

Bwana yake hari muwilini ikamtoka
Arufu nzuri , ya miski humiminika
**Tena hunawiri kama lulu kumemetuka**
Mkono kiweka hubakia arufu njema

Tashibihi zote zilizotumiwa na mtunzi katika ukawafi huu ni mwafaka katika kuelezea maudhui kwani zinatuonyesha uhalisia wa mambo hasa katika umbo la Mtume.

### 3. 2.2 Sitiari

Hii ni mbinu ya matumizi ya lugha ambayo inafumba maana lakini inatilia mkazo jambo linaloelezwa. Katika tamathali hii, vitu viwili vinalinganishwa kwa kutumia kiungo 'ni'. Wamitila (2003) anafafanua sitiari kama ulinganishi ambao hautumii viunganishi vyovyote katika uwasilishaji wake. Hii ni mbinu ambayo hukuza sifa ya ulinganishi kwa kusema kitu fulani ni kingine. Mweri (2010) akitoa mchango wake katika ufafanuzi wa sitiari anasema kuwa hii ni mbinu ya uvunjaji wa kanuni za kisemantiki ambazo hutumiwa na mtunzi katika kazi za kifasihi ili kupitisha ujumbe maalum.

Wa Mutiso (2005) anasema kuwa sitiari ni tamathali ambayo inalinganisha vitu vyenye tabia zinazofanana. Ulinganishi huu wa kitu kimoja na kingine unafanywa bila kutumia viunganishi kama vile: kama, ja, mithili ya na kadhalika. Vitu vinavyounganishwa mara nyingi huwa tofauti kimaumbile na hata kitabia. Kulingana naye tamathali hii hutumiwa kujenga taswira fulani.

Msokile naye (1993) anaunga mkono mawazo ya wataalamu hao kwa kusema kuwa ulinganishi katika tamathali hii hautumii maneno ya viungo kama vile: kana, mfano wa, mithili ya, kana kwamba na kadhalika. Mtunzi hufanya ulinganisho wa sitiari  kwa kufanya kitu kimoja kisemwe

kuwa ni kingine. Kwa mfano nywele za Asha ni kichaka, maisha ni moshi. Hapa mtunzi katika mfano wa kwanza anafananisha wingi wa nywele na kichaka na mfano wa pili anafananisha maisha yanayopita kama moshi.

Tamathali hii hutumiwa ili kujenga taswira akilini mwa msomaji. Hivyo ulinganishi huu si wa moja kwa moja kama ulivyo katika tashbihi. Vitu viwili tofauti kitabia na kimaumbile huhusishwa. Kwa mfano, unapomwita mtu fisi inawezekana akawa anahusika na sifa fulani zinazofanana na mnyama huyo kama vile sifa ya ulafi.

Mtunzi katika ukawafi huu ametumia sitiari katika sehemu mbalimbali. Katika ubeti wa 21, mtunzi anamfananisha Mtume Muhamad na taa ambayo itawaangazia waumini wa jamii ya Makka. Jamii hii kabla ya kuzaliwa kwa Mtume waliabudu masanamu na kushiriki mambo ya uchawi na ushirikina. Tabia hii ilimchukiza Mwenyezi Mungu hivyo akamtuma Mtume kuja kuwakomboa kutokana na kuabudu miungu hiyo. Hivyo akamteua Mtume kuja ulimwenguni kuwafahamisha matakwa ya Mwenyezi Mungu ya kuabudu Mungu wa kweli na mmoja. Ujio wa Mtume duniani ulidhamiria kuwaongoza na kuwaonyesha njia ya kweli. Huyu ni Bwana wa ajabu ambaye atawatoa kwenye ukafiri na kuwaonyesha mwanga.

Bishara kapowa mama yake usingizini,
Kuwa metukuwa mimba yake bwana wa shani,
Naye atakua **taa njema ulimwenguni,**
Walio zizani ukafiri utaongoka
( ubeti wa 21).

Katika kufafanua sura ya Mtume Muhamad, mtunzi anazifananisha nywele zake na singa. Hizi ni nywele ndefu zilizonyooka kama vile za Wazungu, Wahindi na Waraabu. Sitiari hii inatupa taswira ya jinsi nywele za Mtume zilivyochangia uzuri wake. Katika ubeti huo huo mtunzi anatuelezea kuwa ndevu zake nyingi anazifananisha na nyumba ya msonge, (ubeti wa 82).

**Nyushize zifunge nyee zake zali za singa**
Meno pangepange katikayo hutoa yanga
**Ndevu ni msonge pua yake ngwa ya upanga**
Hapana muinga kwa sifaze nilozisema

Mtunzi pia ametumia tamathali ya sitiari katika ubeti wa 25. Hapo anamfananisha Mtume na nyota inayoleta baraka. Dhamira ya mtunzi katika ubeti huu ni kuwa kuzaliwa kwake Muhamad kunadhamiriwa kuleta heri kwa maisha ya wanajamii. Huyu ni mtoto ambaye anafurahiwa na Mwenyezi Mungu na alitumwa ulimwenguni kwa majukumu maalum. Mtume ndiye kitovu cha dini. Hii ni sitiari inayoashiria kuwa Mtume ndiye mwasisi wa dini ya Kiislamu. Mtunzi pia anatuarifu kuwa Mtume ni nyota. Nyota kwa kawaida huwa na mwangaza na huonekena usiku wakati wa giza. Haya ni maelezo yanayopatikana katika ubeti wa 25.

Mahurulaini wote pia walioshuka,
Kutoka peponi ili kwamba kufurahika,
**Kiini kya dini yake jua hapa kimefunuka**,
**Nyota ya Baraka duniani imesimama.**

Katika ubeti wa 7, mtunzi pia ametumia sitiari ambapo anaomba msaada kwa Mwenyezi Mungu ili ajadili maisha ya Mtume katika kuandika ukawafi huu. Anamfananisha Mwenyezi Mungu na nguzo ambayo inatumiwa na watu kuegemea ili wasianguke. Kwa kawaida nguzo ni muhimili wa kutengenezea nyumba. Kulingana na mtunzi hawezi kufanya lolote bila uwezo wa Mwenyezi Mungu, (ubeti wa 7).

T’aka msa’ada wa uwezo wake Jaliya
Kwani hila sina kwa kufanya kwa zote ndiya,
**Kwake Rahamana ndiyo nguzo kutegemeya**,
Wa kuniwezeya kuyatunga maneno mema.

Sitiari hizi zimetumiwa na mtunzi ili kumfanya msomaji afikirie na kujenga taswira fulani akilini mwake.

### 3.2.3 Tashihisi

Kimsingi, tashihisi ni mbinu ya usemi ambayo huwasilisha vitu visivyokuwa na uhai kufanya matendo ya kibinadamu. Wamitila (2003) anaongezea kusema kuwa, katika mbinu hii, mtunzi husawiri vitu visivyokuwa na uhai kupewa sifa za binadamu za kufikiri na kuhisi. Mara nyingi mbinu hii huhusisha wanyama ambao hupewa sifa za binadamu. Tamathali hii hutumiwa na watunzi wa kazi ya kifasihi ili kugusa hisi ya msomaji au msikilizaji.

Msokile (1993) anaongezea katika ufafanuzi huu kwa kusema kuwa, mbali na mbinu hii kuwapa wanyama matendo ya kibinadamu, yeye ametoa mazingira matatu makuu ambayo hutumia sana mbinu hii. Tashihisi ni sitiari ambayo inaeleza kitu kisichokuwa mtu kufanya tabia za mtu. Pia anaifafanua kama sehemu ya umbile la binadamu huchukuliwa na kupewa sifa za binadamu. Aidha ni mbinu ambayo kitu kisicho hai huwasilishwa na kupewa wazo la kiumbe hai.

Maelezo haya yanakubaliana na maoni ya Oriedo (2007) kuwa mbinu hii ya kisanii huipa sifa za kibinadamu kitu kisicho hai. Kwa mfano, 'kifo tafadhali songa mbali'. Katika mfano huu, kifo kimepewa sifa ya kibinadamu ya kutembea na kusonga. Kingei' na Kemoli (2001) wanarejelea mbinu hii kama mbinu ya uhuishaji. Mvati (2009) anakubaliana na wataalamu wengine kuwa mbinu hii huvipa sifa na tabia za kibinadamu vitu ambavyo havina uhai. Sisi pia tunakubaliana na wataalamu hawa kuwa tashihisi ni mbinu ambayo huvipa sifa za kibinadamu viumbe ambavyo havina uhai. Mtunzi katika ukawafi tunaoshughulikia ametumia mbinu hii kukuza utukufu wa Mtume kwa kuhusisha miti, wanyama kufanya shughuli zinazofanywa na watu katika jamii.

Katika ubeti 19 na 20 mtunzi anatuelezea jinsi misitu na wanyama walivyofurahia ujauzito wa Bi Amina akitarajia kumzaa mtume Muhamad.

**Chaka kikaondoka kwa furaha yake hashimu,**
**Na yake Baraka miti yote ikawa tamu**,
**Na nyama kuteka kwa fasaha kutakalamu**,
**Wote masanamu walo yuu wakainama.**
( ubeti 19)

Katika ubeti huu miti inaonekana ikibarikiwa na kichaka kikapata miguu na kuondoka sehemu kilipokuwa awali ishara ya kufarahia kwa ujio wa Mtume duniani. Hapa miti imepewa sifa ambazo kwa kawaida haziwezi kufanya ila binadamu pekee. Mtunzi anatuarifu kuwa wanyama pia walicheka na kuzungumza, hali ambayo kwa kawaida haiwezi kutokea kwani wanyama hawawezi kuzungumza na kucheka kama binadamu.

Majini ni viumbe visivyoonekana, si shetani wala pepo lakini watu huamini kuwa yapo duniani. Majini yanaweza kusababisha furaha na hata huzuni. Katika ubeti wa 20, mtunzi amewapa viumbe hawa uwezo wa kibinadamu wa kuzungumza na kuwaonya makuhani wa uongo kuhusu Mtume aliyetarajiwa kuleta dini ya kweli. Mtunzi ametumia mbinu hii ili kukuza dhamira yake.

**Wakamba majinni ya wakati wa kurubiya**,
Wote makuhani ya wurongo watazuwiya,
Hapa duniyani na furaha ikaeneya,
**Sasa amekuya bwana wetu wa mila mema.**
( ubeti 20).

Mtunzi katika ubeti 44 anatuarifu jinsi miti ilivyosujudu mbele ya Mtume alipoenda Syria na ami yake bwana Abu Talib kwa shughuli za kibiashara. Kwa kawaida miti haiwezi kuinama na kusujudu kama anavyofanya binadamu. Mtunzi ametumia tamathali hii ili kusisitiza ukuu wa Mtume Muhamad.

Bahira kanena arudishe kijana kyake,
**Mti nimeona husujudu kwa mbee yake,**
Wala sijaona illa kuwa ni T'umwa wake
Heri endazake mayahudi si watu wema
( ubeti 44).

Mtume alipofikisha miaka ishirini na mitano pia alienda safari ya kibiashara huko Basra ambapo palikuwa na mansura mmoja aliyeshuhudia kivuli cha mti kilivyomuinamia Mtume. Hili ni dhihirisho kuwa mtunzi amefanikisha kututhibitishia na kutuonyesha kuwa Mtume Muhamad ndiye aliyeteuliwa na Mola kuja kuwaokoa viumbe wote walioko duniani. Hivyo hata mimea ilitambua ukuu wake, (ubeti 46).

Na ya pili mara umriwe t'aubaini,
Kwa kwenda Basora ni hamsa wa ishirini,
Upo mansura papo hapo kwa tayakini

**Kiketi mtini kivulikye kikainama.**

Mtunzi wa maulidi ya *jambeni* amefanikiwa kutumia mbinu hii ya tashihisi ili kuipa kazi yake uhai.

### 3. 2.4 Chuku

Katika mbinu hii, mtunzi anakuza sifa ya kitu fulani kuliko kawaida. Hii ni mbinu ambayo hutilia mkazo, ukubwa au udogo kwa kiasi kikubwa ambapo masuala fulani katika kazi ya kifasihi yanachimuzwa. Wamitila (2003) anaiita mbinu hii udamisi. Njogu na Chimerah (1999) wanaifafanua tamathali ya chuku kama mbinu ya kutia chumvi ili kueleza jambo fulani kwa msisitizo. Kwa mfano, mtu anaposema kuwa siku hizi sili kwa kukutamani. Huwa anasisitiza jinsi anavyompenda msikilizaji wake lakini ukweli ni kuwa kumpenda mtu hakuwezi kumzuia mtu mwingine kula**.**

Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* mtunzi ametumia mbinu hii ili kukuza uzuri na sifa za Mtume Muhamad. Mtunzi anaeleza umbo la Mtume Muhamad na anakiri kwamba hakuna maneno mwafaka yanavyoelezea uzuri wa umbo la Mtume Muhamad. Hii ni chuku kwani amekuza uzuri huu kupita kawaida kuwa alikuwa na sifa nyingi na hakuna anayeweza kuziandika zote au kuzitaja zote, ( ubeti 85).

**Hapana muweza swifa zake kuziandika,**
**Zote kumaliza au mwenye kuzitamuka,**
Nililoliweza tabaruku ili kutaka,
Kwa yake Baraka tumwa wetu wa sifa njema.

Katika ubeti wa 84, mbinu ya chuku pia imetumiwa na mtunzi ambapo anatuarifu kuwa jasho lake Mtume likitoka hutoa harufu nzuri sana ya manukato na anang’aa sana, (ubeti 84).

Bwana yake hari muwilini ikamtoka
**Arufu nzuri ya misiki humiminika**
Tena hunawiri kama lulu kumemetuka
**Mkono kiweka hubakia arufu njema**

Katika ubeti 83, mtunzi anasema:

**Kifua kipana nyee zake hutiririka**,
Sikio la bwana kwa ukuu hufunikiwa,
Uso wa mungwana una nuru hunawirika,
**Kitwa kutukuka kwa akili ndio alama.**

Sehemu hizi za mwili wa Mtume zimekuzwa kupita kawaida, kila sehemu ina jukumu lake linalopasa kutekeleza. Lakini sehemu za mwili wa Mtume, licha kuwa na majukumu yake ya kawaida, mtunzi amezipa sehemu hizo majukumu ya ziada. Kichwa chake kuwa kila wakati kinatukuka kwa sababu ya akili nyingi alizo nazo.

Katika safari ya mtume kwenda Madina, mtunzi katika ubeti wa 78 anatuarifu kuwa njiani alikutana na Bi. Umma Maabadi ambaye mbuzi wake hakuwa na uwezo wa kutoa maziwa lakini Mtume alipofika na kumgusa chuchu zake alitoa maziwa mengi wakanywa na kujaza vyombo vyote vilivyokuwapo. Hii ni chuku kwani ni nadra sana mbuzi kutoa maziwa mengi hadi vyombo vyote vilivyoko nyumbani vijae vyote. Mtunzi alitaka kusisitiza jinsi mbuzi huyo alivyotoa maziwa mengi sana.

Kwa Baraka njema kapapasa kiwele kyake,
**Tumwa akakama yakatosha maziwa yake,**
**Zombo zikakoma zikayaa zilizo kwake**,
Kwa mkono wake wa Baraka wenye karama.
( ubeti 78)

Mtunzi katika ubeti wa 29 ametumia chuku kwa kutuarifu jinsi Mtume Muhamad alivyokuwa alipozaliwa. Anatudokezea kuwa, Mtume alizaliwa akiwa safi kwani sehemu zake za siri zilikuwa zishatahiriwa na kitovu kishakatwa. Kauli hizi zinakuza sifa zake kuwa yeye alikuwa mtoto tofauti na watoto wengine ambao lazima watahiriwe baada ya kuzaliwa.

Kazawa Rasuli unadhifu ulikuwa,
Hitani ya kweli akitoka ametahiriwa,
Kitovu kamili kimekatwa akizaliwa,

Na wetu Moliwa kwa kudura yake Rahma,
( ubeti 29).

### 3.2.5 Takriri

Kimsingi takriri ni marudio ya neno, sauti, herufi au wazo katika kazi ya kifasihi. Hii ni tamathali ambayo hutumiwa na mtunzi kurejelea urudiaji wa sauti fulani. Urudiaji huu hufanywa kimaksudi ili kusistiza jambo. Wamitila (2003, 2004, 2008), anasema kuwa takriri zinaweza kuwa za aina mbalimbali. Kuna takriri irabu, takriri konsonanti, takriri silabi, takriri mzizi, takriri neno, takriri mistari na takriri wazo.

Mbali na aina hizi za takriri, pia anafafanua takriri ya kimuundo kama urudiaji ambapo muundo fulani wa kishazi au sentensi unarudiwarudiwa katika sehemu fulani za kazi ya kifasihi. Takriri hii hutumiwa na mtunzi wa kazi ya kifasihi ili kusisitiza ujumbe wake na kuendeleza maudhui aliyonuia kuyawasilisha. Mtaalamu huyu anaifananisha dhana hii na istilahi ya usambamba ambayo pia inahusu urudiaji wa sehemu maalum za sentensi au virai.

#### 3.2.5.1 Takriri Irabu

Takriri irabu ni urudiaji wa sauti ya irabu katika sehemu sawa za neno katika sentensi. Mtunzi anaweza kurudia irabu kimaksudi ili kupata wizani na ridhimu fulani katika kazi yake, (Wamitila, 2008). Katika ubeti wa 1, irabu **u** imerudiwarudiwa:

Nanda kwandika kwa yinalo Mwenye Hishima,
**U**liyetukuka zilo k'uu zako ne'ema,
**U**siye na shaka kwa umoya na udaima,
**U**liye Karima kwa zipowa zako na'ima.
( ubeti 1).

Mtunzi amerudia irabu '**u**' katika mianzo ya sentensi hizo ili kupata ridhimu na kusisitiza ujumbe wake ambao ni ukuu wa Mungu.

Mifano mingine ya takriri irabu inajitokeza katika ubeti wa 40 ambapo mtunzi anarudia irabu '**a**' ili kusisitiza ujumbe wake.

Yalipotimiya  myaka mine umri wake,
**A**lishika ndiya kasafiri naye mamake,
**A**ka azimiya munawari ili wafike,
Kirudi mamake ikawele ndiyo hatima.
(ubeti wa 40).

Takriri hii imetumiwa ili kusisitiza safari waliyokuwa nayo Bi. Amina na mtoto wake Mtume. Hivyo irabu **a** imerudiwa katika mianzo ya sentensi ya pili na ya tatu kutilia mkazo ujumbe huo.

Katika ubeti wa 95, mtunzi pia ametumia takriri irabu ambapo anarudia irabu '**u'** katika kuwasilisha ujumbe wake.

Mengi nimewata kwa urefu nimecheleya,
**U**zito kusita kwa zijana kuhafifiya,
**U**kitoa sit azote pia zitatimiya,
Kuwa mia moya baitize zitatimama.
( ubeti wa 95).

Irabu **u** imerudiwa ili kusisitiza dhamira ya mtunzi kuwa hangeweza kuendelea kuandika zaidi na amewacha mambo mengi kwa kuwa hakutaka kuurefusha sana utungo wake.

### 3.2.5.2 Takriri Konsonanti

Takriri konsonanti ni urudiaji wa sauti ya konsonanti. Urudiaji huu mara nyingi hutokea mwanzoni mwa sentensi lakini pia mtunzi anaweza kutumia mahali pengine popote katika kazi yake, ( Wamitila 2003). Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni*, takriri konsonanti  imejitokeza katika ubeti wa 78, ambapo konsonanti **z** inarudiwarudiwa ili kuunda wizani maalumu na kusisitiza ujumbe wake katika sentensi hiyo, ( ubeti 78).

Kwa Baraka njema kapapasa kiwele kyake,
Tumwa akakama yakatosha maziwa yake,
**Z**ombo **z**ikakoma **z**ikayaa **z**ilizo kwake,
Kwa mkono wake wa Baraka wenye karama.

Katika mshororo wa tatu, mtunzi amerudia konsonanti '**z'** ili kusisitiza ujumbe kwa wasomaji wake.

Mtunzi pia katika ubeti wa 82 ametumia takriri konsonanti ili kusisitiza uhalisia wa sehemu za mwili wa Mtume Muhamad. Konsonanti **ng** imerudiwa kufafanua zaidi ndevu na pua yake.

Nyusize zifunge nyee zake hutiririka,
Meno pangepange katikayo hutoa yanga,
Ndevu ni mso**ng**e pua yake **ng**wa ya upa**ng**a
Hapana muinga kwa swifaze nalozinena.
( ubeti 82).

Mtunzi amerudia konsonanti **ng** kusisitiza ujumbe kwa kuonyesha uhalisia wa umbo la Mtume Muhamad.

**3.2.5. 3 Takriri Silabi.**

Huu ni urudiaji ambao hutokea kwa wingi katika kazi za kishairi. Katika urudiaji huu silabi za aina moja zinajitokeza katikati au mwishoni mwa mshororo. Takriri hii huwa na muungano wa konsonanti na vokali na hutokea kuwa vina vya kila ubeti. Ifuatayo ni mifano katika ubeti wa 76, ambao kina cha kati '**ri'** na kina cha mwisho '**na'** kimerudiwarudiwa ili kupata ulinganishi wa vina.

Katika safa**ri** ya mtume kwenda Madi**na**
Hao makafi**ri** kukwandama wakayane**na**
Surata wa he**ri** ni mtume wakaona**na**
Yahaki kaona nyama wake alipozama
( ubeti 76)

Silabi **ri** na silabi **na** katika ubeti huu zimerudiwa ili kupata urari wa vina vya ukwapi na vina vya mwandamizi mtawalia.

Mifano mingine ya beti yenye takriri silabi ni :

Kija Jiburi**li** kwa utumwa wa Mola wa**ke**
Hata kwa Rasu**li** nali hali yu pweke ya**ke**

Katika jaba**li** li Hiraa mahala pa**ke**
Ili itamuke ikira'a kwa kuisoma
( ubeti 57)

Akapanda Bwa**na** mbingu zote pasi na sha**ka**
Mitumi kuo**na** waloyuwa wakatamu**ka**
Wote wakine**na** na Mtumi kufurahi**ka**
Ndiye wa baraka ulokuya ndiye hatima
( ubeti 66)

Mifano hii pia ni dhihirisho la kuonyesha vina vya ukwapi na vina vya mwandamizi ndivyo vinavyofanana lakini vina vya utao havifanani katika kila ubeti. Silabi hizi zimetumiwa ili kupatanisha vina katika ukawafi huu wa *Maulidi ya Jambeni.* Hivyo ukawafi huu una muundo ufuatao:

__________6a_________4___________5b
__________6a_________4___________5b
__________6a_________4___________5b
__________6c_________4___________5d

Muundo huu unadhihirisha kuwa takriri silabi imetumika katika ukawafi wote kuanzia mwanzo hadi tamati. Muundo huu unaonyesha kuwa silabi za vina vya ukwapi katika ubeti mmoja vinafanana na silabi za vina vya mwandamizi pia vinalingana. Kila ubeti una vina vyake vya kipande cha ukwapi na kipande cha mwandamizi vinavyofanana lakini ambavyo vinatofautiana na beti zingine. Muundo wa 6-4-5 unamaanisha kuwa, katika kila mshororo, kipande cha ukwapi kina mizani 6, kipande cha utao kina mizani 4 na kipande cha mwandamizi kina mizani 5. Takriri hii imetumiwa na mtunzi ili kupata urari wa vina na pia kupata wizani maalumu katika shairi hilo.

Mbali na kuonyesha urari wa vina vya ukwapi na mwandamizi, takriri silabi pia imetumiwa na mtunzi katika ubeti wa 74. Mtunzi anatufahamisha kuwa Makureshi walipotaka kumuua Mtume,

Mwenyezi Mungu alimwagiza ahame na kwenda Madina. Mtume alifuata agizo hilo na mara moja akahama, dini hiyo ilienea sana Madina.

T'umwa akatoka kwa amri yake Moliwa
Akagura Maka na Madina akapokewa,
Dini katukuka ndi**po** ha**po** ili**po**kuwa
Na wote wakawa makafiri kurudi nyuma.
(ubeti 74)

Silabi **po** imerudiwa katika sentensi hii ili kuleta mvuto na wizani katika matamshi.

### 3.2.5. 4 Takriri Mzizi

Takriri mzizi ni aina ya takriri ambapo mzizi wa neno unarudiwa ili kurahisisha matamshi. Katika ukawafi huu, mzizi **tak** umerudiwa katika maneno tofauti katika sentensi moja. Takriri hii imejitokeza katika ubeti wa 67.

Akisikiya Arishini kwa Mola wake,
Akakurubiya kama kandu na kaba yake,
Mola kamwambiya u**tak**alo kwangu u**ta**ke,
Wewe ndiwe pweke niloumba mbingu Hashima.

Mtunzi amerudia mzizi **tak** katika mshororo wa tatu ili kutia mkazo jambo analolizungumzia.

### 3.2.5. 5 Takriri Neno

Takriri neno ni urudiaji ambapo mtunzi wa kazi ya kisanaa hurudiarudia maneno fulani ili kuleta msisitizo. Urudiaji huu hufanywa ili kuleta mhimizo fulani katika matini ya mtunzi. Katika ubeti wa 82, mtunzi ametumia takriri neno ili kusisitiza umbo la mtume Muhamad akifafanua jinsi meno yake yalivyo, ( ubeti wa 82).

Nyusize zifunge nyee zake hutiririka,
Meno **pangepange** katikayo hutoa yanga,
Ndevu ni msonge pua yake ngwa ya upanga,
Hapana muinga kwa swifaze nalozinena.

Aidha katika ubeti wa 36 mtunzi pia ametumia takriri neno ili kusisitiza dini ambayo Mtume aliileta baada ya kuzaliwa yaani dini njema ambayo itaondoa dini ya makafiri ambayo inapoteza watu. Katika ubeti wa 36 mtunzi anarudia neno dini ili kuleta msisitizo wa dini hizi mbili.

Mwingi wa fahari alizawa Mfungo-sita,
Ni alifajiri na wakati sitowasita,
Ithina'ashari Makafiri wakaikuta,
Ikakutakuta **dini** mbovu kwa **din**i njema.
( ubeti 36)

Katika ubeti wa 45, mtunzi pia anatumia takriri neno ambapo anasisitiza jinsi Mtume na Maisari walivyopewa mali na Bi. Khadija ili waende kufanya biashara. Hii ilikuwa mara yake ya pili kwa Mtume kwenda safari za kibiashara tangu alipoajiriwa na Bi. Khadija. Kwa uaminifu wake alichaguliwa na Bi. Khadija kuwa mumewe, katika ubeti wa 45, mtunzi anasema, '**akampa'** mali na **'akampa'** Maisari. Mtunzi anasisitiza jinsi Bi. Khadija alivyovutiwa na Mtume kwa uaminifu wake, hivyo akampa mali na Maisari kuandamana naye.

Vile vile mtunzi ametumia takriri neno katika ubeti wa 66, wakati Mtume alipopanda hadi mbingu ya saba ili kuonana ana kwa ana na Mola wake. Kitendo hiki kiliwafurahisha mitume wengine wa awali waliomtangulia Mtume Muhamad. Baadhi ya mitume hao wa awali ni mtume Ibrahimu, mtume Issa na wengine. Wote walikiri kuwa Muhamad ndiye mtume wa mwisho na wa baraka, ( ubeti wa 66), " **ndiye** wa Baraka alokuya **ndiye** hatima". Neno **ndiye** limerudiwa ili kusisitiza kuwa Mtume ndiye wa haki na kweli na pia wa mwisho.

Takriri neno pia imejitokeza katika ubeti wa 50 ambapo Bi. Khadija alisadiki kuwa Mtume Muhamad ndiye aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu. Hii ni baada ya kuona ishara ambazo zilijitokeza katika maisha ya Mtume Muhamad. Katika ubeti wa 50, mtunzi anasema, ' kwa kuona alama **zake** akazaa zijana **zake'**. Mtunzi ametumia takriri ili kusisitiza ishara alizoziona Bi. Khadija na kusadiki kuwa Mtume ni mtu wa kipekee tofauti na watu wengine.

### 3.2.5.6 Takriri Wazo

Msokile (1993) amefafanua takriri wazo kuwa ni aina ya urudiaji ambapo mawazo fulani yanarudiwa kutoka ubeti hadi ubeti kwa lengo la kusisitiza ujumbe. Katika ubeti wa 21 na 26 maneno **Bwana wa shani** yametumiwa:

Bishara kapowa mama yake usingizini,
Kuwa metukuwa mimba yake **Bwana wa shani,**
Naye atakuwa Taa njema ulimwenguni,
Walio zizani ukafiri utaongoka.
( ubeti 21)

Na alipozawa mwenyi yina **Bwana wa shani**
Kitwa meinuwa kiekeza kuko mbinguni
Ili kumuyuwa walioko ulimwenguni
Kwamba yake dini na ukuu mbwake daima
( ubeti 26)

Mtunzi amerudia maneno **Bwana wa shani** katika beti hizi mbili ili kusisitiza upekee wa Mtume kuwa ni kiumbe wa ajabu.

Vile vile, mtunzi ametumia takriri wazo katika ubeti wa 30 na 84 ambapo anasisitiza harufu nzuri ya manukato ambayo Mtume anaitoa kutoka mwilini mwake. Harufu hii ya manukato ilianza kumtoka pindi tu Mtume alipozaliwa. Mtunzi ametumia takriri hii ili kukuza ukuu wa Mtume katika dini ya Kiislamu kuwa ni kiumbe aliyeteuliwa kwa jukumu maalum.

Alipozaliwa T'umwa wetu mwenye baraka,
Wanda ametiwa nazo nuru kumemetuka,
**Harufu kutowa** zilo njema zilizotoka,
Bwana aso shaka ni Mtumi asio shaka.
( ubeti 30)

Bwana yake hari muwilini **ikimtoka,**
'**arufu** nzuri ya misiki humiminika,

Tena hunawiri kama lulu kumemetuka,
Mkono kiweka hubakia ‘arufu njema.
( ubeti 84).

Mtunzi amerudia **harufu iliyomtoka** Mtume mwilini kwa nia ya kusisitiza ujumbe. Mtunzi wa *Maulidi ya Jambeni* amefaulu katika matumizi ya takriri ili kufanya ukawafi huu kuwa wa kuvutia na kunata makini ya wasomaji wake.

### 3.2. 6 Taharuki

Mvati (2009) anafafanua mbinu hii ya taharuki kuwa ni tamathali ambayo mtunzi huonyesha kutoelezea alichotaka kusema mpaka mwishoni mwa shairi lake. Wamitila (2003) kwa upande wake anasema kuwa taharuki kuwa ni istilahi inayotumiwa na mtunzi kuonyesha hamu anayokuwa nayo msomaji yakutaka kujua yatakayotokea. Hali hii humfanya msomaji kutaka kujua mambo ambayo yatatokea baadaye. Hii ni mbinu ambayo humfikirisha msomaji. Katika ubeti wa 64, mtunzi anatufahamisha kuwa Mtume alipofika Makadasi msikitini, mitume wengine walishuka, ( ubeti 64).

Akisa kufika Makadasi msikitini,
Mtumi kashuka wakatoka wote mbinguni,
Amri katoka wakaswali ra’ateni,
Na wetu Amini akwekwa kuwa imama.

Katika ubeti huu, hali ya taharuki ilidhihirika kwani hawakubaini ni mtume yupi atakayeongoza swala kati yao kwani wote walikuwa na uwezo wa kuongoza.

## 3.3 Jazanda / Taswira

Hii ni mbinu ya lugha ambayo hutumiwa kuelezea hasa sifa za matumizi ya picha kwa ujumla wake. Taswira ni mbinu inayotumiwa ili kuelezea neno, kirai au maelezo yanayounda picha fulani katika akili ya msomaji. Picha hizi huundwa kutokana na matumizi ya tamathali zingine kama vile tashbihi, sitiari na mbinu zingine, (Wamitila 2003). Mtunzi ametumia mbinu hii ili kuleta uhalisia na kuendeleza dhamira na maudhui makuu ambayo ni dini, miujiza na ushujaa.

Mulokozi na Kahigi (1979), wanasema kuwa taswira ni mbinu ya tamathali ambayo mara nyingi mtunzi hutumia picha katika utungo wake. Msomaji hujenga picha akilini mwake mtunzi

anapoteuwa maneno yake kwa uangalifu na dhahiri ili kujumuisha na kuhusisha dhana mbalimbali. Kwa upande wao, Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa mbinu hii ya usemi hutumika ili kuvuta picha akilini mwa msomaji. Mbinu hii humwezesha msomaji kuona, kusikia, kuonja, kunusa, kupenda, kuchukizwa na hata kudharau kilichosawiriwa na mtunzi kutegemea nguvu za taswira zilizotumika.

Msokile (1993) katika mchango wake anafafanua taswira kama mkusanyiko wa picha ambazo msanii anaziunda kutokana na maelezo yake katika kazi ya fasihi. Mbinu hii aghalabu hujengwa kutokana na jinsi mtunzi anavyotumia tamathali zingine za usemi hasa sitiari na tashibihi. Mtunzi pia katika kujenga taswira anaweza kutumia ishara mbalimbali ambazo zina mawazo, dhana, vitu na maumbile mbalimbali zinazomfanya msomaji apate hisi za kunusa, kuona, kugusa, kuonja na kusikia.

Wamitila (2004, 2008), anaainisha jazanda katika makundi mawili makuu. Kulingana na mtaalamu huyu, kuna jazanda ya kimaelezo na jazanda ya kiishara. Jazanda ya kimaelezo ni aina ya jazanda ambayo huundwa na msikilizaji au msomaji wa kazi ya kifasihi kutokana na maelezo ya mtunzi. Mara nyingi, mtunzi anapoeleza mtu, mahali au mandhari fulani, msomaji hujenga picha kutokana na maelezo hayo. Mtunzi wa ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* ametumia aina hii ya jazanda katika kuwasilisha dhamira yake. Jazanda ya kiishara kwa upande mwingine ni ile picha ambayo huundwa akilini mwa msomaji lakini picha hizo huwa na maana nyingine za ziada.

Binadamu ana hisia mbalimbali ambapo hisia hizi humsaidia kuunda picha mbalimbali anaposoma kazi za kifasihi. Wamitila (khj) ameainisha taswira zinazolenga kuchochea, kutazama, kunusa, kuonja, kusikia na kadhalika. Msingi huu unatuainishia aina saba za taswira. Hizi ni taswira za harufu zinazojengwa na viungo vinavyohusu harufu. Kwa mfano, mtunzi anapozungumzua kuhusu kinyesi. Msomaji anapata picha ya harufu ya kinyesi hicho. Taswira ya mguso huunda picha ya kugusa kitu au vitu fulani kugusana. Taswira za muonjo hutokana na picha ambazo msomaji hupata hisia za kuonja mtunzi anapozungumzia chakula.

Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni,* mtunzi ametumia kauli mbali mbali zinazojenga taswira tofauti tofauti. Katika ubeti wa 21, mtunzi anatuarifu kuwa mimba ya Bi Amina ilitarajiwa kuleta mtoto ambaye mtunzi anamfananisha na taa njema. Taa hutumiwa kuleta mwangaza katika mazingira mbalimbali. Hivyo anatupa picha ya jinsi Mtume atakavyowaongoza na kuwaelekeza wanajamii kwa kuwatoa katika giza la kutokuwa na dini ya sawa, (ubeti wa 21).

Bishara kapowa mama yake usingizini,
Kuwa metukuwa mimba yake Bwana wa shani,
Naye atakua **Taa njema ulimwenguni,**
Walio zizani ukafiri utaongoka.

Katika ubeti huu, msomaji anapata picha ya jinsi Mtume atakavyowaelekeza na kuwafunza ili kuepukana na maovu ya shetani.

Taswira nyingine inajitokeza wakati Mtume alipopanda hadi mbingu ya saba katika safari yake ya ajabu aliyotumia mnyama buraki. Mtunzi anatuelezea mazingira aliyoyaona alipoenda peponi na pia motoni. Katika mazingira ya peponi mtunzi anatufahamisha kuwa Mtume aliona mahurulaini, wanawake mabikira ambao wamewekewa wanaume wanaoishi maisha ya kitakatifu duniani. Siku ya kiama wanaume hawa watastarehe kwenye mabustani yaliyonadhifishwa vizuri wakiwa na wanawake hao. Maelezo haya yanapatikana katika ubeti wa 68.

**Akenda peponi akaona mambo mazuri,**
**Mahurulaini nguo zao ni za Hariri,**
**Na mabusutani zimo ndani kwa kusawiri**,
Nda watu wa heri Tumwa wetu walomwandama.

Ubeti huu unatupatia picha ya watu walio na furaha na starehe zote waliotenda mambo mazuri tu ya kumpendeza Rabbana walipokuwa duniani. Mtunzi pia anatuarifu kuwa mahurulaini walikuwa wamevaa nguo nzuri za Hariri. Kauli hii inatuonyesha taswira ya wanawake warembo na wakuvutia.

Mtunzi pia anatupa picha ambapo Mtume alitembelea Jahanamu ambapo alikutana na watu wakipigwa na kutaabika wakitokwa na usaha kwenye vichwa vyao. Hawa ni watu ambao

walikataa kufuata maagizo ya Allah walipokuwa duniani na kumfuata shetani. Maelezo haya yanatupa picha ya jinsi mambo yatakavyokuwa ukimuasi Mwenyezi Mungu. Watu hao watakuwa na maisha ya shida na taabu nyingi.

**Kenda na motoni Jahanamu kuimulika,**
**Zigongo zitwani na wasaa kuturuzika,**
**Wao hawasoni siku zote kutaabika,**
Ndio walotaka kumwandama yeye Rajima.
( ubeti 69).

Taswira pia inajitokeza wakati mtunzi anatufafanulia umbo na sura ya Mtume Muhamad. Ametumia mbinu mbalimbali kutuchorea picha kamili ya umbo lake. Rangi ya mwili wake anatufahamisha ni mweupe wenye wekundu uliokolea, mrefu kiasi kwa kimo, macho yaliyopakwa wanda, meno yenye mwanya, ndevu nyingi, pua iliyonyoka, nywele ndefu za singa na kifua kipana. Maelezo haya yanamfanya msomaji wa ukawafi huo kupata picha maalum na kuona jinsi Mtume alivyokuwa katika umbo lake la kimwili. Haya ni maelezo yanayopatikana katika ubeti wa 81, 82, 83

Tumwa namswifu alomwema sura tabiya,
**Mweupe sharifu wekunduni imengilia,**
**Kimo kya urefu na matoni wanda katiya,**
Sikukusudiya memtia Mola karima.
( ubeti 81).

**Nyusi zifunge nyee zake zali za singa,**
**Meno pangepange katikayo kutoa yanga,**
**Ndevu ni msonge pua yake ngwa ja upanga,**
Hapana muinga kwa swifaze na alozisema.
(ubeti 82).

**Kifua kipana nyee zake hutiririka,**
Shikio la bwana kwa ukuu hufunikika,
Uso wa mungwana una nuru hunawirika,
**Kitwa kutukuka kwa akili ndiyo alama**.
( ubeti 83).

Picha nyingine imejitokeza ambapo mtunzi ametufahamisha matukio ya kimuijiza ambayo yalitokea wakati Mtume alipozaliwa. Katika ubeti wa 25, mtunzi anatuelezea kuwa baadhi ya wakunga waliompokea Mtume alipokuwa anazaliwa walikuwa mahurulaini wanaoishi peponi ambao walishuka kuja kumlaki Mtume duniani. Hivyo msomaji anapata taswira ya jinsi viumbe hawa walivyoshuka na kuja kumlaki Mtume, ( ubeti wa 25).

**Mahurulaini wote pia walioshuka,**
Kutoka peponi ili kwamba kufurahika,
Kiini kya dini yake jua hapa kimefunuka,
Nyota ya Baraka duniani imesimama.

Mtunzi anatuchorea picha katika ubeti wa 26 ambapo Mtume aliinua kichwa pindi tu alipozaliwa. Dhamira ya tukio hili lilikuwa ni kuonyesha ukuu wa Mtume Muhamad na kuwa yeye ni tofauti na watoto wengine katika jamii. Mtunzi amefanikiwa kutuonyesha kuwa mtoto Muhamad atapaa hadi ngazi za juu jambo ambalo lilitokea baadaye katika maisha yake. Haya ni maelezo ambayo yanajitokeza katika katika ubeti wa 26.

Na alipozawa mwenyi yina Bwana wa shani,
**Kitwa meinua kiekeza kuko mbinguni,**
Ili kumuyua walioko ulimwenguni,
Kwamba yake dini na ukuu mbwake daima.

Taswira nyingine inadhihirika katika ubeti wa 29 ambapo mtunzi anatuelezea jinsi Mtume alivyozaliwa akiwa tayari ameshapashwa tohara pia kitovu chake kimeshakatwa. Kwa kawaida mtoto hutahiriwa ili kumzuia uambukizi wa magonjwa lakini kwa sababu ya utakatifu wa Mtume yeye alizaliwa kama sehemu zake za siri zimeshatahiriwa. Kitovu husaidia mtoto kupata chakula kutoka kwa mama yake mzazi akiwa tumboni. Mtume alipata chakula akiwa tumboni moja kwa moja kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mtunzi ametumia taswira hii ili kuwasilisha utakatifu wa Mtume Muhamad. Mtunzi anatuchorea picha ya mtu safi. Sio kama watoto wengine ambao lazima watahiriwe ndipo wasafishwe.

Kazawa Rasuli unadhifu ulikuwa,
**Hitani ya kweli akitoka ametahiriwa,**
**Kitovu kamili kimekatwa akizaliwa,**
Na wetu Moliwa kwa kudura yake Rahma,
( ubeti 29).

Mtume pia alizaliwa akiwa amepakwa wanda. Wanda hupakwa watoto wachanga ili kuwazuia kutokana na kijicho cha wanajamii. Hii ni kutokana na mila na desturi za jamii. Ulinzi wa Mtume ulitoka kwa Mola kwani hakukuwa na mwanadamu ambaye angeweza kumdhuru Mtume. Mtunzi pia anatufahamisha kuwa Mtume alipozaliwa nuru iliangaza kuashiria ufanisi ambao wanajamii wataupata kutokana na kuzaliwa kwake. Maelezo haya yanapatikana katika ubeti wa 30.

Alipozaliwa Tumwa wetu mwenye Baraka,
**Wanda ametiwa nazo nuru kumemetuka,**
**Harufu katoa zilo njema zilizotoka,**
Bwana asoshaka ni mtumi asiyoshaka.

Ubeti huu unatupa picha ya mtoto aliye imara na thabiti ambaye hakuna kiumbe yeyote ambaye anaweza kumdhuru kwa hali yoyote hapa duniani.

### 3.4 Lakabu

Hii ni mbinu ya lugha ambayo mtunzi wa kazi ya kifasihi anawapa majina ya badia baadhi ya wahusika wake kulingana na sifa zao, ( Msokile 1993). Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* mtunzi katika kukuza sifa za Mtume Muhamad ambaye ndiye mhusika mkuu wa kazi hiyo, ametumia jina la kilakabu ili kupata taswira yake kamili.

Mtume Muhamad kwa uaminifu wake alipewa jina la Al- amin. Hili ni jina linalopewa watu waaminifu wanaoaminiwa na watu wengi katika jamii. Katika ubeti 55 mtunzi anatueleza jinsi Mtume alivyohukumu vyema wakati Makureshi walipotaka kurudisha lile jiwe jeusi lililoko kwenye kaaba lilipovunjwa na mafuriko huko Makka. Alitoa uamuzi uliomtuliza kila mtu ambaye alitaka arudishe jiwe hilo la kaaba. Katika ubeti wa 51 tunaambiwa:

Nyaka katimiya T'umwa wetu mwenye imani,
Haya nisikiya ni hamsa wa thalathini,
Yalowangiliya kuraishi yao shidani,
**Na yeye Amini kahukumu hukumu njema.**

Katika ubeti 64 na 65, pia mtunzi anatuelezea kitendo ambacho alifanya alipoenda Makadasi msikitini huko Jerusalem katika safari yake ya kwenda hadi mbingu ya saba. Hali hii ilitokana na uaminifu wake na utiifu wake kwa Mwenyezi Mungu kwani pindi tu Jibril alipomhakikishia kuwa Mola wake alimtaka arishini mwake alienda bila kusita, ( ubeti 64).

Amri katoka wakaswali raka' ateni,
**Na wetu Amini akawekwa kuwa imama**.

Kwishakwe kuswali ikashuka ngazi mbinguni,
**Kaya Jiburili kamwambia wetu Amini**.
( ubeti 65).

### 3.5 Visawe

Mbinu hii hutumiwa na mtunzi wa kazi ya kifasihi kuelezea neno ambalo lina maana sawa na neno lingine, (Wamitila, 2003). Hutumiwa ili kupunguza urudiaji wa neno moja kila wakati na kuonyesha sifa mbalimbali. Mtunzi wa ukawafi huu ametumia visawe kurejelea mhusika Mtume na mhusika Allah. Katika ubeti wa 6 ametumia neno **Mola, Jalia**, ubeti wa 7 ametumia neno **Rahamana**, ubeti wa 28 ametumia neno **Jabbaru**, ubeti wa 29 ametumia neno **Rahima**. Maneno haya yametumiwa kumrejelea Mwenyezi Mungu ili kuonyesha sifa zake mbalimbali. Maneno ya visawe aliyotumia mtunzi akimrejea Mtume ni **Rasuli, Mtumwa** na **Mungwana.**

### 3.6 Matumizi ya Nahau na Misemo

Wamitila (2003), amefafanua nahau kama misemo inayofafanua maana iliyofichika. Kulingana naye, nahau ni misemo ya picha ambayo huwa na undani wa maana kuliko misemo

inayopatikana katika lugha fulani. Mara nyingi nahau huundwa na kitenzi na jina. Baadhi ya nahau ni kuasi ukapera, ikimaanisha kuoa, kaza kamba, maana yake ni kuongeza juhudi na kadhalika.

Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni,* mtunzi ametumia misemo na nahau katika kuwasilisha ujumbe wake. Katika ubeti wa tano, ametumia kauli ambayo maana yake imejificha ambayo msomaji inampasa afikirie. Anadokeza kuwa anaomba Mwenyezi Mungu amuongoze kufuata *njia ya haki.* Mtunzi ametumia kauli 'njia ya haki' kumaanisha kuwa Mola amjalie kufuata dini ya kweli.

Nakuomba Mola nifuate **ndiya ya haki,**
Ndiyo njema mila aloyenda alo swadiki,
Nisiwe na 'ila linenwalo lisiwe dhiki,
Yote na hakiki zilo kweli hadithi njema.
( ubeti 5).

Katika ubeti wa 37, mtunzi anatufahamisha mwaka aliozaliwa Mtume Muhamad. Anauhusisha mwaka huo na mwaka wa ndovu ambapo ndovu waliingia mji wa Makka. Kauli hii inatoa maana ambayo inamfanya msomaji kuhusisha mwaka ambao Mtume alizaliwa, na mwaka ambao watu walikuja kutaka kuuchukuwa kwa nguvu na kuutawala mji wa Makka lakini hawakufaulu,
( ubeti wa 37).

**Ni mwaka wa ndovu walotaka kungia Makka,**
Na watu waovu walokuya ili kuteka,
Ndio wapumbavu hija njema ilikunduka,
Kwa yake Baraka wakawele kurudi nyuma.

Aidha katika ubeti wa 40, mtunzi anasema:

Yalipotimiya myaka minne umri wake,
**Ashika ndia** kasafiri naye mamake,
Akazimika mnawazi ili wafike,
Kurudi mamake ikawele ndio hatima.

Shika njia' ni msemo ambao unamaanisha kuwa mama yake Mtume Bi. Amina alifunga safari na kwenda Madina. Mtunzi ametumia misemo kwa lengo la kupamba kazi yake. Hii ni mbinu inayotumiwa na mtunzi kwa nia ya kusitiri maana na kumfanya msomaji kutafakari ujumbe.

Katika ubeti 82, mtunzi ametumia misemo kufafanua umbo la mtume Muhamad. Anafafanua jinsi nyusi zake zilivyo, nywele, ndevu zake na hata pua yake.

**Nyusize zifunge** nyee zake hutiririka,
Meno pangepange katikayo hutoa yanga,
Ndevu ni msonge **pua yake ngwa ya upanga**,
Hapana muinga kwa swifaze nalozisema.
( ubeti 82) .

Mtunzi ametumia misemo hii ili kurembesha lugha yake, kusisitiza na kuleta uhalisia wa umbo la Mtume katika kukuza maudhui ya kidini.

### 3.7 Uhuru wa Kishairi

Mbatiah ( 2001) anasema kuwa uhuru wa kishairi una maana mbili tofauti lakini zinazohusiana Kwanza anafafanua dhana hii kama hali ambapo mtunzi anakiuka sheria za namna anavyotumia lugha katika viwango vya sarufi, msamiati, sintaksia na hata semantiki. Maana ya pili ni ukiukaji wa kaida za kijamii. Mtunzi wa kishairi ana uhuru wa kutumia lugha namna anavyotaka ilimradi asipoteze maana anayodhamiria katika kazi husika.

#### 3.7. 1 Ukiushi wa Kisintakisia

Wamitila (2003) anasema kuwa ukiushi wa kisintakisia hutokea wakati ambapo mtunzi anaandika sentensi zinazokiuka miundo ya lugha iliyozoeleka katika fasihi ya Kiswahili. Ukiushi huu unajikita katika mpangilio wa maneno katika sentensi. Mtunzi ana uhuru wa kutofuata sheria za sarufi ili apate ukamilifu wa vina na mizani. Aina hii ya ukiushi inahusishwa pia na mbinu ya tabdila ambapo mtunzi anawasilisha neno tofauti na vile lilivyo kihalisia ili apate urari wa vina katika kazi yake.

Mtunzi katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* ametumia ukiushi wa aina hii ili kupata urari wa vina. Mtunzi amelazimika kubadilisha miundo ya baadhi ya virai katika utungo wake ili kutimiliza arudhi zinazomfunga katika ukawafi huu. Katika ubeti wa 23, mtunzi anabadilisha muundo wa sentensi ili apate kina cha mwisho ambacho ni **li**, ( ubeti 23).

Na ilipotimu mimba yake myezi miwili
Baba wa Hashimu **ilikuja yake ajali**
Ni mwezi timamu wa maradhi yalowaswili
Muyea Rasuli  alikufa bwanetu mwema

Katika mshororo wa pili amesema **ilikuja yake ajali** badala ya **ajali yake ilikuja**.

| **Mifano ya ukiushi** | **muundo halisia** | **ubeti** |
|---|---|---|
| Wote mahasidi | mahasidi wote | 22 |
| Kwamba yake dini | kwamba dini yake | 26 |
| Na wetu Moliwa | Na Moliwa wetu | 29 |
| Wanda ametiwa | Ametiwa wanda | 30 |
| Kwa wetu nabiya | kwa nabiya wetu | 34 |
| Manuwari ili afike | ili afike manuwari | 40 |
| Makka akangiya | akaingiya Makka | 48 |
| Hira akinenda | akinenda Hira | 56 |
| Kumwambia wetu Amini | kumwambia Amini wetu | 65 |

Mtunzi ametumia ukiushi huu wa kisintakisia ili kupata urari wa vina na ukawafi wake uwe na mdundo maalum kwa nia ya kupamba ukawafi huu.

### 3.7.2 Ukiushi wa Kisemantiki

Wamitila (2003) anafafanua ukiushi huu kuwa aina ya uhuru ambapo mtunzi wa kazi ya fasihi anazua dhana ambazo zina maana isiyo ya kawaida. Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* mtunzi ametumia ukiushi huu kwa kuvipa vitu visivyo na uhai sifa za kibinadamu. Ukiushi huu

humsaidia mtunzi kuipa kazi yake uhai. Katika aina hii ya ukiushi mtunzi anaeleza dhana fulani kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kawaida katika jamii. Mtunzi wa ukawafi tunaoushughulikia ametumia kwa kiasi kikubwa aina hii ya ukiushi ili kuipa kazi yake uhai. Katika ubeti wa 46, mtunzi anatufahamisha kuwa, Mtume alipoenda safari ya kibiashara huko Basra, Mansura aliona kivuli cha mti kikiinama, ( ubeti wa 46).

Na ya pili mara umriwe t'aubaini,
Kwa kwenda Basora ni hamsa wa 'ishirini,
Upo mansura papo hapo kwa tayakini,
**Kiketi mtini kivulikye kikainama.**

Katika mshororo wa nne mti umepewa uhai kwa kuweza kuinama na kumfunika Mtume kitendo ambacho hakiwezekani kwa kawaida. Wanadamu ndio wenye uwezo wa kuinama. Mtunzi alitumia ukiushi huu ili kukuza ukuu wa Mtume Muhamad kama kiongozi wa dini ya Kiislamu.

### 3.7.3 Ukiushi wa Kimofolojia

Wamitila, ( 2003) anaeleza kuwa ukiushi huu hujitokeza katika uendelezaji wa maneno. Huu ni ukiushi ambao unahusu aina tatu wa kimofolojia ambazo ni: inkisari, tabdila na mazida. Mtunzi ana uwezo wa kubadilisha muundo wa sarufi ili kupata urari wa vina na mizani. Mtunzi anaweza fikia malengo haya kwa kurefusha neno, kufupisha au kubadilisha maendelezo ya neno. Tumezifafanua aina hizi za ukiushi wakati tumechambua uhuru wa mshairi katika kupata vina na mizani maalum katika kazi yake.

#### 3.7.3.1 Inkisari

Kimsingi ni mbinu ya kufupisha maneno ili kupata utoshelevu wa mizani. Wamitila (2003) anaifafanua dhana hii kama njia ya mkato inayohusiswa sana na ushairi. Ili kupata utoshelevu wa vina na mizani, mshairi ana uhuru wa kutumia mbinu hii ili kupata idadi maalumu ya mizani. Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni,* mtunzi ametumia mbinu hii ili kuwasilisha dhamira yake.

**Mifano ya maneno yaliyofupishwa katika *Maulidi Ya Jambeni***

| | | |
|---|---|---|
| T'aka | Nataka | 7 |
| Alotutoleya | Aliyotutoleya | 18 |
| Chaka | Kichaka | 19 |
| Bwanetu | Bwana wetu | 22 |
| Waloandama | Walioandama | 24 |
| 'meinuwa | Ameinuwa | 26 |
| Zilo | Zilizo | 30 |
| Aso | Asiye | 30 |
| Walo | Walio | 32 |
| Maziwaye | Maziwa yake | 38 |
| Lilo | Lililo | 39 |
| Nyama | Mnyama | 39 |
| Walokonda | Waliokonda | 39 |
| Mamake | Mama yake | 40 |
| Make | Mama yake | 41 |
| Babake | Baba yake | 43 |
| Kenda | Akaenda | 43 |
| Akangiya | Akaingia | 43 |
| Kamuona | Akamuona | 43 |
| Umriwe | Umri wake | 46 |
| Kwaye | Kwake yeye | 47 |
| Mefunikwa | Amefunikwa | 48 |
| Mkwewe | Mkwe wake | 59 |
| Kwishakwe | Kwisha kwake | 65 |
| Niloumba | Niliyeumba | 67 |
| Nyusize | Nyusi zake | 82 |
| Hisabuye | Hisabu yake | 93 |

### 3.7.3. 2 Tabdila

Mbinu hii imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali. King'ei na Kimoli, ( 2001) wanafafanua dhana hii kama mbinu inayotumiwa na mtunzi kwa kubadilisha tahajia za maneno lakini ubadilishaji huo haurefushi wala kufupisha mizani. Lengo kuu la tabdila ni kupata urari wa vina. Wamitila (2008) anaitaja mbinu hii kama mbinu inayobadilisha uendelezaji wa maneno na kumwezesha mtunzi kufuata kaida za kiarudhi za kupatikana kwa mizani au kina fulani katika kazi ya fasihi.

Katika ukawafi tulioshughulikia, mtunzi ametumia mbinu hii katika sehemu nyingi kwa madhumuni tuliyoyataja. Katika ubeti wa 94, mtunzi ametumia neno '**timama'** badala ya neno **'timamu',** neno '**imama'** badala ya '**imamu'** ubeti wa 64, neno ,'**karima'** badala ya '**karimu,'** ubeti wa 60. Haya ni maneno ya mwisho katika kipande cha mwandamizi katika mshororo wa nne katika ukawafi huo. Mtunzi ametumia kina '**ma'** katika kila mshororo wa nne wa kipande cha mwandamizi isipokuwa ubeti wa 16, 21 na 30 peke yake.

Akapata shida T'umwa wetu akisimama,
Wapije shahada masanamu kuyasukuma,
Washike ibada aloyeta Mola Karima,
Kulla mtu mwema kaongoka na kumuanda**ma**.
( ubeti 60).

.

Akisa kufika Makadasi msikitini,
Mtumi kushuka wakitoka wote mbinguni,
Amri katoka wakaswali raka'ateni,
Na wetu Amini akawekwa kuwa ima**ma**.
( ubeti 64).

Na yangu kabila ni Bakari kuifahamu,
Alonipa mola kazaliwa nt'I ya Amu,
Ndiyo yangu mila ya mtumi mwenye hishimu
Nisake timamu zake swifa zilo tima**ma**.
( ubeti 94).

Hizi ni beti ambazo mtunzi amebadilisha mwendelezo wa maneno ili kupata ulinganishi wa vina vya mwandamizi katika mishororo hiyo.

Mifano mwingine wa tabdila umejitokeza katika ubeti wa 94 ambapo mtunzi anatumia neno '**hishimu'** badala ya '**hishima** ili kupata kina **mu** badala ya **ma.** Mtunzi ametumia mbinu hii ili kupata urari wa vina katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* na pia kuipa kazi yake sura ya kishairi.

### 3.7.3. 3 Mazida

Oriedo (2007) anaitaja mbinu hii kama uhuru wa mtunzi ambapo anarefusha maneno anayotumia katika shairi lake ili kupata upatanisho wa vina na mizani. Maneno haya hurefushwa kwa kuongezea silabi bila kubadilisha maaana ya maneno hayo. Katika ukawafi tunaoshughulikia, mtunzi ametumia mbinu hii katika beti mbalimbali ili kupata idadi ya mizani zinazotakikana na pia urari wa vina kwa nia ya kupamba kazi yake. Katika ubeti wa 4, mtunzi anatumia neno '**wafuatee'** ambalo lina mizani 5 badala ya '**wafuate**' lenye mizani 4, ( ubeti 4).

Radhi nakuomba ya ilahi iwashukie
Zijana za nyumba ya Mtume iwaenee
Swahaba naomba na wengine **wafuatee**
Radhi uwawie hawa wote wenye hishima

Ubeti wa 91 mtunzi ametumia mazida katika neno '**nitolikoma'** badala ya '**nilikoma'** pia ili kupata idadi kamili ya mizani. Ukiushi huu umetumiwa na mtunzi ili kupata ukamilifu wa mizani katika ukawafi huu.

## 3.8 Sajili ya Lugha

Wamitila ( 2008) anasema kuwa jinsi lugha inavyotumiwa katika jamii hutofautiana kulingana na mazingira na muktadha wa watumiaji wake. Huu ndio msingi wa rejesta za lugha ambazo sifa zake kuu zinatokana na muktadha wa mazungumzo. Odeo na Maliachi (2008) wanafafanua sajili ya lugha kama matumizi mbalimbali ya lugha moja.

Sajili hutegemea sheria za mazingira, wahusika kwa kuangazia umri wao, hadhi zao n.k. Kaida hizi hutoa mamlaka ya jinsi lugha itakavyotumika kwa kufuata mtindo fulani. Kuna sajili za aina mbalimbali kama vile sajili ya kibiashara, sajili ya kidini, sajili ya maongezi ya kawaida na kadhalika. Sajili hizi zinabainishwa na sifa maalumu zinazowaongoza watumiaji wake katika kuteua aina fulani ya msamiati, maneno, miundo na maudhui.

Mtunzi anapoandika kazi yake ya kifasihi ana uwezo wa kukiuka sifa za sajili mahususi au akachanganya sajili mbalimbali hivyo kuibuka na mtindo changamano wa mawasiliano. Uteuzi wa maneno kimuktadha, ni kipengele muhimu cha lugha ambacho huweza kuikuza dhamira ya mtunzi kwa kiasi kikubwa. Kwa kuwa lugha ni nyenzo kuu ya kukuza na kuendeleza maudhui, ni muhimu mtunzi kuwa na sajili moja kuu inayotawala kazi husika na kama atachanganya sajili nyingine basi atumie kwa kiwango kidogo. Sajili inayotawala kazi itadhihirishwa na uteuzi wa msamiati, tamathali zinazotumiwa na motifu. Mtunzi wa *Maulidi ya Jambeni* ametumia lugha ya sajili ya maabadini.

### 3.8.1 Sajili ya Maabadini

Odeo na Maliachi (2008) wanasema kuwa maabadi ni sehemu ambayo hutumiwa na waumini wa dini fulani ili kumtukuza Mola wao. Mahali hapa paweza kuwa kanisani, msikitini au mahali maalumu palipotengwa ili kumtukuza Mwenyezi Mungu . Shughuli za ibada zinaweza kutokea mahali popote pawe uwanjani au chini ya mti bora pametengwa kwa nia hiyo. Wataalamu hawa wanatoa sifa mbalimbali za maabadani.

#### 3.8.1.1 Sifa za sajili za Maabadani

Sajili ya maabadani huwa na sifa ambazo zinatofautisha lugha inayotumiwa katika sehemu hiyo na sehemu nyingine yoyote katika jamii. Baadhi ya sifa za sajili ya Maabadani ni:

##### 3.8.1.1.1 Uteuzi wa Msamiati Maalumu

Kazi za kidini hutumia msamiati mahususi katika uwasilishaji wake. Mtunzi wa kazi za kidini hutumia lugha sahili ili kueleweka na waumini wa dini hiyo. Msamiati unaotumika mara nyingi huwa ni wa kumsifu Mwenyezi Mungu na shujaa wa dini husika. Kila dini ina maneno maalumu

ambayo hayatokei katika muktadha mwingine. Kwa mfano neno Allah linahusishwa tu na dini ya Kiislamu wala si dini nyingine. Jina Mtume kumrejelea Muhamad pia linahusishwa na Kiislamu. Dini zingine zina majina yao maalum ambayo ni tofauti.

Mtunzi wa *Maulidi ya Jambeni* ametumia majina maalumu ya kumtaja Mwenyezi Mungu kulingana na sifa zake. Kwa mfano ametumia neno Rahima kuashiria rehema na huruma zake. Majina mengine ni Mola, Jalia, Rahamana na Jabbaru. Huu ni msamiati maalumu ambao aghalabu hutumiwa katika muktadha wa dini ya Kiislamu. Aidha, ili kurahisisha mawasiliano na uelewa wa ujumbe, mtunzi ametumia kahaja ya Kiamu.

Katika kauli za kumsifu Mtume, mtunzi katika ubeti wa 24 na 73 anamtaja Mtume kama mtu Mungwana. Mungwana ni mtu mwenye adabu na desturi njema. Mtu anayekaa na binadamu wenziwe kwa uzuri. Mtu Mwenye utu. Hili ni jina la heshima analoitwa mtu mwenye sifa hizo. Mtunzi amempa Mtume jina hilo kwa sababu ya sifa zake njema, ( ubeti 24).

Yalipotimia mimba yake wetu **mungwana**,
Ni myezi tisiya alizaa mwana Amina.
( ubeti 24).

Wote anusari wanawake hata zijana,
Wakamhitari kumwandama wetu **mungwana.**
**(** ubeti 73).

Katika ubeti wa 31 mtunzi anamtaja Mtume Muhamad kuwa kiumbe mwenye kipawa na uwezo wa namna ya kipekee. Yeye ana uwezo wa kuomba haja kwa Mwenyezi Mungu na kukubaliwa mara moja. Pindi tu Mtume alipozaliwa, mtunzi alifahamu kuwa atakuwa na uwezo huo. Hivyo anatumia neno la mtu mwenye ‘karama’ ili kufanikisha dhamira ya kumkuza na kumtukuza Mtume wa Mwenyezi Mungu. Maelezo haya yanapatikana katika ubeti wa 31.

Baada ya kuzawa, zilitoka nyingi ajabu
Ili kumuyuwa Maajamu na Waarabu

Wakaziwiliwa mashetani wasijaribu
Mambo ya ghalibu kwa kuzawa mwenye **Karama**

Pia katika ukawafi huu, mtunzi ametumia kauli za kumtukuza Mwenyezi Mungu kwani yeye ndiye mwenye wema wote na huruma. Katika ubeti wa 60, mtunzi ametumia neno 'Karima',ambalo linamfafanua mhusika Allah kama mwenye sifa za ukarimu. Mtu karimu ni mtu mwenye moyo wa kutoa kitu kumpa mtu mwingine bila ya kuwa na choyo na kufanya ubahili. Huyu ni mwenye kupenda sana kutoa au kusaidia kwa hali na mali. Sifa hii imetumiwa na mtunzi ili kudhihirisha wema wa Allah kwa wanadamu wote duniani, (ubeti 60).

Akapata shida Tumwa wetu akasimama
Wapige shahada masanamu kuyasukuma
Washike ibada aloyeta Mola **Karima**
Kulla mtu mwema kaongoka na kumwandama

**3.8.1.1.2 Matumizi ya Lugha ya Kuogofya na Lugha ya Matumaini**

Tungo za kidini huwa na sifa ya kutumia lugha ya kuogofya kwa waumini wake ili kuwafahamisha hatima ya maisha yao baada ya kuondoka duniani. Kauli hizi huwasaidia waumini kuishi maisha ya kumpendeza Mwenyezi Mungu ili waweze kupata thawabu katika ulimwengu wao wa pili. Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni*, mtunzi anatuarifu hali aliyokumbana nayo alipotembezwa Jahanamu kwa kuona watu wakipigwa na kutaabika.

Kenda na motoni Jahannamu kuimunika,
Zigongo zitwana na wasaa kuturuzika,
Wao hawa soni siku zote kutaabika,
Ndiyo walotaka kumwandama yeye Rajima.
( ubeti 69).

Vilevile, katika ukawafi huu, mtunzi anawatia moyo waumini wa dini hii kwa kuwahimiza waishi maisha ya kumcha Mwenyezi Mungu ili wakitoka duniani wakastarehe na Mola wao. Mtumzi katika ubeti 68, anatuarifu kuwa Mtume alipoenda peponi aliwapata mahurulaini, wanawake mabikira ambao huwekewa wanaume wanaoishi maisha matakatifu duniani.

Mandhari ya sehemu hiyo pia yamenadhifishwa vizuri na mabustani kuhifadhiwa. Kauli hii inawatia moyo waumini na kuwapa tumaini la maisha mema ya baadaye.

Akenda na p'eponi akaona mambo mazuri,
Mahuri layini nguo zao ni za Hariri,
Na mabusutani zimo ndani kwa kusawari,
Nda watu wa heri T'umwa wetu walomwandama.
( ubeti wa 68).

#### 3.8.1.1. 3 Matumizi ya maneno ya kigeni

Kazi za kifasihi zinazohusu maswala ya kidini hutumia maneno ya kigeni ambayo ndiyo asili ya dini hiyo. Kila dini ina asili yake na vitabu vitakatifu vya kila dini viliandikwa kwa lugha asilia. Tungo za kidini huwa na majina ya kigeni ya wahusika wake, maeneo na hata matukio ya zamani. Ni rahisi kutambua tungo zilizoandikwa kwa muktadha wa kidini kwa matumizi maalumu ya maneno ili kuelimisha, kuonya, kushawishi, kuamuru na kuelekeza kauli fulani. Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* Mtunzi ametumia maneno mengi ya Kiarabu. Mifano ya baadhi ya maneno hayo ni Rajima katika ubeti wa 69, Rasuli, ubeti wa 29, rakaa, ubeti wa 64, imamu, ubeti wa 64, alifu, ubeti wa 93, kaaba, ubeti wa 63, arsh, ubeti wa 67, thenashara, ubeti wa 43, shahada, ubeti wa 60, hijra, ubeti wa 93 na mengi mengineyo.

## 3.9 Dhima ya Matumizi ya Lugha katika Kuwasilisha Dhamira na Maudhui katika *Maulidi ya Jambeni*

Lugha aliyotumia mtunzi imemsaidia kwa kiwango kikubwa kufanikisha dhamira na maudhui makuu ambayo ni dini, ushujaa na miujiza. Mtunzi katika kutumia tamathali mbalimbali ameweza kurahisisha mawasiliano, kuipamba lugha na kuhamasisha jamii lengwa na kadhalika.

### 3.9.1 Kupamba Lugha

Ili kuwasilisha ujumbe wake, mtunzi hutumia lugha ili kumfanya msomaji awe na hamu ya kutaka kuendelea kuisoma kazi hiyo. Hivyo hulazimika kutumia viungo mbalimbali vinavyoipa ladha kazi husika. Katika *Maulidi ya Jambeni* mtunzi amefanikiwa kutumia tamathali

mbalimbali ili kuipamba lugha yake katika ukawafi huo. Ametumia tashibihi, sitiari, chuku na tashihisi. Lengo lake kuu lilikuwa ni kuonyesha jinsi Mtume alivyoteuliwa na Mwenyezi Mungu ili kuwaokoa wanajamii kutokana na dhambi. Kwa mfano katika beti hizi:

Akapanda bwana mbinu zote pasi na shaka
Mitumi kuona waloyua wakatamuka
Wote wakinena wa mtumi kufurahika
**Ndiye wa Baraka ulokuya ndiye hatima**.

**Nyusize zifunge nyee zake zali za singa**
**Meno pangepange katikayo hutoa yanga**
**Ndevu ni msonge pua yake ngwa ja upanga**
Hapana muinga kwa swifaze nalozisema

Katika beti hizi mbili mtunzi ametumia lugha ya kitamathali ambapo msomaji anavutiwa kwanza na umbo la mtume na pia anapata uhalisia na picha kamili. Tamathali hizi humfanya msomaji kuwa na hamu ya kutaka kuendelea kusoma ukawafi husika. Katika ubeti wa kwanza mtunzi ametumia mbinu ya sitiari kufafanua baraka alizo nazo Mtume na ubeti unaofuata ametumia sitiari na tashibihi ili kuifanya lugha yake iwe na mvuto kwa wasomaji.

### 3.9.2 Kufanikisha Mawasiliano

Lugha ndio nyenzo kuu ya mawasiliano katika kazi yoyote ya kifasihi. Mtunzi katika *Maulidi ya Jambeni* ametumia lugha ya lahaja ya Kiamu ili kufanikisha mawasiliano kwa hadhira lengwa. Ukawafi huu umejikita katika maswala ya kidini hasa dini ya Kiislamu. Hivyo ili kurahisisha mawasiliano ametumia lugha ya Kiarabu na lahaja ya Kiamu ikizingatiwa kuwa dini hii inahusiana sana na Kiarabu. Hii ni kwa sababu kitabu kitakatifu cha dini hii yaani Quran kimeandikwa kwa lugha hiyo. Dhamira ya mtunzi ni kuwaelimisha wanajamii hasa wafuasi wa dini ya Kiislamu kufahamu maisha ya shujaa wao wa kidini ambaye alipewa zawadi ya Quran takatifu ili kuwaelekeza katika kuabudu Mungu mmoja. Mtunzi amefanikiwa kutumia lahaja ya Kiamu na maneno ya Kiarabu ili kuwasilisha dhamira hiyo.

### 3.9.3 Kufafanua Jambo

Tamathali za usemi zilizotumiwa na mtunzi katika ukawafi huu zilikuwa na dhima kuu ya kufafanua maswala muhimu ya kimaudhui. Mtunzi katika kuwasilisha maudhui ya kimuijiza ametumia lugha ya kitamathali ambapo mambo ya kimiujza yamewasilishwa ili kuleta uhalisia katika maisha ya Mtume. Misemo iliyotumiwa pia imemfafanua Mtume kwa uwazi.

Katika ubeti wa 25, mtunzi anatuonyesha tukio la kiajabu ambapo mahurulaini, viumbe waishio peponi, walivyoshuka kumlaki Mtume ambaye mtunzi anamfananisha na nyota ya baraka. Katika ubeti huu mtunzi anatumia sitiari hiyo kutupa uhalisia wa mandhari yalivyokuwa wakati Bi Amina alipokuwa akijifungua. Tukio hilo linadhihirisha kuwa Mtume alikuwa mtoto wa kipekee ambaye aliletwa duniani kwa jukumu la kuwaokoa wanajamii.

### 3.9.4 Kuhamasisha Jamii

Lugha ya kitamathali iliyotumika katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* imetumiwa na mtunzi ili kuhamasisha jamii. Uhamasishaji unahusu kitendo cha kuitaka jamii kufanya jambo na kuacha kufanya jambo jingine kwa nia ya kuepuka madhara. Dhamira kuu ya mtunzi ni kuwafahamisha waumini wa jamii ya Kiislamu na wengine kufahamu umuhimu wa Mtume Mohammad ambaye ni shujaa wa dini hiyo na jinsi alivyotetewa kutokana na mikono katili ya Makureshi. Mtume aliletwa duniani kuwaongoza na kuwaelekeza wanajamii kutoka kuabudu masanamu ili waabudu Mungu mmoja. Mtunzi ametumia tamathali mbalimbali kwa lengo la kukuza ushirikiano na udugu wa jamii katika dini.

### 3.9.5 Kumfikirisha Msomaji

Tamathali za usemi zimetumiwa na mtunzi kwa dhima ya kumfanya msomaji afikirie zaidi kuhusu ujumbe unaowasilishwa. Hizi ni mbinu muhimu za kumshirikisha msomaji katika kazi maalumu. Mtunzi katika *Maulidi ya Jambeni* amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutumia lugha ya kitamathali kumshirikisha msomaji kwa kutumia mbinu anuai. Mbinu ya matumizi ya taswira katika ukawafi huu imemsaidia msomaji kutafakari na kufikiria hali halisi ya jinsi ujumbe ulivyojitokeza, kwa mfano mtunzi alipoeleza taswira ya jehanamu katika ubeti wa 69. Ubeti huu unaonyesha hali halisi ya mandhari ya kutisha kwa wale waliomuasi Mola walipokuwa duniani.

Msomaji anapata wasaa wa kutafakari maisha ya anasa za dunia ambazo mwisho ni moto wa milele.

### 3.9.6 Kusisitiza Uthabiti wa Ujumbe Unaowasilishwa

Mtunzi wa kazi ya kifasihi hutumia lugha ya kitamathali katika kazi yake kwa lengo la kusisitiza uthabiti wa ujumbe anaouwasilisha kwa wasomaji wake. Matumizi ya tamathali za usemi huongeza nguvu za ujumbe kuaminika zaidi kwa hadhira inayokusudiwa kupata ujumbe huo. Mtunzi wa *Maulidi ya Jambeni* ametumia semi hizi ili kusisitiza ukweli wa dhamira yake katika kazi yake. Semi  nyingi amezitumia kufafanua sifa za Mtume na umbo lake ili hadhira ipate uhalisia wa picha kamili ya Mtume Muhamad.

### Hitimisho

Katika sura hii tumehakiki matumizi ya lugha katika Ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni*. Tumechambua tamathali za usemi alizotumia mtunzi ili kukuza maudhui yake. Aidha tumejadili lahaja na sajili iliyojikita katika ukawafi huu. Vile vile tumeangazia ukiushi wa kishairi aliotumia mtunzi kwa madhumuni kadhaa. Tumebaini umuhimu wa kutumia lugha ya kitamathali katika kazi ya kisanaa. Lugha aliyotumia mtunzi imefanikisha kazi yake.

## SURA YA NNE

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumetoa hitimisho la utafiti wetu ambao ulishughulikia uchambuzi wa matumizi ya lugha katika Ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni.* Nadharia ya umuundo ndiyo iliyotuongoza katika kufanya utafiti. Mtunzi amefanikiwa pakubwa kwa kuteua maneno ya kuvutia na yenye mnato ili kuendeleza dhamira na maudhui yake. Pia tumetoa mapendekezo.

### 4.1 Muhtasari wa Utafiti

Katika sura ya kwanza tumeshughulikia maswala ya kimsingi yanayojenga utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali tuliyonuia kuyajibu katika utafiti wetu, sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada yetu na njia za utafiti.

Maswali tuliyonuia kuyajibu katika utafiti wetu ni yafuatayo; swali letu la kwanza la utafiti lilikuwa ni: mbinu za matumizi ya lugha zilizotumiwa na mtunzi ili kuendeleza maudhui na dhamira yake  katika Ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni* ni zipi?. Swali la pili lilikuwa, uteuzi wa mbinu hizi za matumizi ya lugha zimechangia vipi katika kuleta ufanisi wa uwasilishaji wa dhamira katika *Maulidi ya Jambeni?.*

Katika sura ya pili, tumetoa muhtasari wa ukawafi huu kwa kuangazia maisha ya Mtume tangu alipozaliwa hadi alipopata utume na kwenda Madina kueneza dini. Katika sura hii pia tumetoa msingi wa uhakiki wa kifani katika fasihi. Tumefafanua vipengele vya kifani vinavyotumiwa na mtunzi katika kazi ya kisanaa. Baadhi ya vipengele vya kifani tulivyovichanganua ni muundo, mtindo na matumizi ya lugha.

Katika sura ya tatu, temehakiki matumizi ya lugha. Tumefafanua baadhi ya vipengele vinavyochunguzwa katika uhakiki wa mgao huu wa fani. Lugha ndiyo malighafi inayotumiwa na mtunzi ili kutoa mawazo yake kwa hadhira. Katika sehemu hii, tumechambua  tamathali za usemi kwa undani huku tukibaini jinsi zinavyojitokeza katika kuendeleza maudhui  makuu

ambayo ni dini, miujiza na ushujaa katika *Maulidi ya Jambeni.* Baadhi ya tamathali tulizojadili ni tashibihi, sitiari, chuku  tashihisi, takriri na taharuki, ambazo ni kiungo muhimu katika kazi yoyote ya kifasihi. Mtunzi wa kazi husika hutumia lugha ya kitamathali ili kuipamba na kusisitiza ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Aidha tumehakiki  sajili iliyomwongoza mtunzi katika kuwasilisha ujumbe wake. Mwandishi hana budi kutumia msamiati kulingana na muktadha. Sajili ya lugha humuongoza mtunzi kuteua miundo ya maneno ambayo yanawiana na muktadha husika. Vile vile, tumeangazia lahaja iliyotumiwa ili kurahisisha mawasiliano katika jamii inayozungumza lahaja hiyo. Tumechambua jinsi lahaja hiyo ilivyojitokeza katika ukawafi huo na mchango wake katika kuwasilisha dhamira kuu. Mwisho tumetoa dhima ya tamathali za usemi katika kazi ya kifasihi. Tumebaini kuwa matumizi ya tamathali ni muhimu katika kufafanua mambo yanayozungumziwa, hutumiwa kusisitiza ujumbe. Tamathali pia ni muhimu katika kumhusisha msomaji katika kazi ya kifasihi kwani humfanya afikirie maana ya dhana zilizotumiwa ambazo zina maana fiche.

## 4.2 Mapendekezo

Katika ukawafi wa *Maulidi ya Jambeni,* tumechambua matumizi ya lugha. Katika uchambuzi huu, tumehakiki tamathali za usemi zilizojitokeza katika ukawafi huu na mchango wake katika kuendeleza maudhui ya kidini na ushujaa. Aidha, tumeangazia dhima za tamathali hizi katika kazi nzima. Tumejadili sajili ya lugha iliyotumika ili kumuongoza mtunzi katika kuteua msamiati wake. Tunapendekeza watafiti wengine waangazie vipengele vingine vya kifani kama vile wahusika, mandhari, msuko  na muundo katika ukawafi huu. Pia tunapendekeza watafiti wa baadaye wachanganue maudhui yanayojitokeza katika ukawafi huu.

**MAREJELEO**

Al-Farsy, A. S. (1974) *Qurani Takatifu.* Nairobi: Islamic Foundation Publishers.

Faki, M. (2015) "Kuchunguza Sifa za Kifani za Utendi wa Kiswahili*; utendi wa Fumo Liyongo.* Dar es Salaam. Chuo cha Huria.

Ferdinard, S ( 1959) *Course in General Linguistics*. New York: Mc Graw-Hill Book Company.

Lugwiri, P. (2011) "Sitiari, Taashira na Tashbihi katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka"* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

Karanja, M. (2014) "Matumizi ya Istilahi na Tashbiha katika *Diwani ya Sauti ya Dhiki*" Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa ).

King'ei, K na Kemoli, A (2001) *Taaluma Ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Kipacha, A. ( 2003) *Lahaja za Kiswahili.* Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Huria.

Kisilu, P. (2003) "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia" Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

Knappert, J. (1971) *Swahili Islamic Poetry Vol 111: Miraj and Maulid*, E. J. Brill: Leiden.

Kofa, T. ( 2006) "Fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

Kombo, M. ( 2014) "Tamathali za Usemi katika Mashairi ya Magazetini: Uchunguzi wa Kifani wa Mashairi ya Ukimwi". Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Huria, ( Haijachapishwa ).

Mbatiah, M. (2002*). Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mgullu, R. ( 1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mnyampala, M. (1965) *Diwani ya Mnyampala.* Dar es Salaam: EALB.

Msokile, M. ( 1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Muchiri, A. (2016) "Fani Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii."* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. ( Haijachapishwa).

Mukuthuria, M. (2007) 'Upekee wa *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*: Utenzi wa Mpito, Mseto Wa Imani za Jadi na Usasa'. 16 (3): 298-319 ( 2007).

Mulokozi, M. (1996) *Fasihi ya Kiswahili:* Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Huria

Mulokozi, M. na Kahigi, K. ( 1979) *Kunga Za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar es Salaam. TPH.

Mungai, P. ( 2005) "Ulinganishi wa Kifani wa *Tenzi* za *Swifa ya Nguvumali na Mikidadi na Mayasa."* Tasnifu ya Uzamili Chuo cha Kikuu Nairobi. ( Haijachapishwa).

Mvati, na Wenzake ( 2009) *Nuru Ya Ushairi :* Nairobi: KLB.

Mweri, G. ( 2010) *Utangulizi Wa Isimu:* Nairobi. KLB.

Mwilaria, R. (2011) "Fani katika *Utenzi wa Ayub*" Tasnifu ya Uzamili Chuo Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Ndumbu, K. ( 2013) "Matumizi ya Takriri na Sitiari katika *Utendi wa Rasil- Ghuli*." Tasnifu ya Uzamili Chuo cha Nairobi, ( Haijachapishwa).

Njogu, K. na Chimerah, R . (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Wafula, R.. (2007). *Nadharia za uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyonje, J na Habwe, J. (2007) *Darubini ya utunzi- insha na Tungo Amilifu za Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Ntarangwi, M. ( 2004) "Uhakiki wa Kazi za Fasihi". Tasnifu ya PHD Chuo Kikuu Augustana: Rock Island, IL 61201.

Obuchi, S. na Mukhwana, A. ( 2015) *Muundo Wa Kiswahili Ngazi na Vipengele*. Nairobi: JKF

Odeo, I. na Maliachi, G. (2008), *Fani ya Isimu Jamii kwa Shule za Sekondari.* Nairobi :Oxford University Press.

Omari, M. ( 2010) "Uchambuzi wa Tamathali za Usemi pamoja na Mbinu Nyengine za matumizi ya Lugha katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Nairobi ( Haijachapishwa ).

Omwoyo, O. (1997) "Fani katika Ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega: Uhakiki wa *Upisho wa Malenga na Dafina ya Malemga".* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Nairobi, ( Haijachapishwa).

Oriedo, E. (2007) *Istilahi za Fasihi ya Kiswahili:* Nairobi: KLB

Senkoro. K. (1982) *Ushairi, Nadharia na tahakiki*. Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press.

Somo na Wenzake, ( 2011) *Sauti ya Shangwe*.Mombasa: Chesil Printers.

Soud, Z. ( 2016) " Fani Katika *Maulidi ya Nuni"* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Nairobi. ( Haijachapishwa).

Wamitila, K. W. (2002*). Uhakiki wa Fasihi : Misingi na Vipengele vyake* .Nairobi: Phoenix publications .

___________ (2003*). Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus

Publication L.t.d.

__________(2004). *Kichocheo cha Fasihi; Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publictions L.t.d.

__________(2008). *Kanzi ya Fasihi:* Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Nairobi Vude Muwa Publishers Ltd.

Waititu, F. na Ipara, I. ( 2006) *Kiswahili Fasaha Kidato Cha 4:* Nairobi Oxford University Press.

Wa Mutiso, K. ( 2005) *Utenzi wa Hamziyah*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Dar es Salaam.

Wesa, R (2005) "Uhakiki wa Kifani katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*". Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Nairobi, (Haijachapishwa).